# Nipashe

Alhamisi Aprili 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580565

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





**Wadau tiba waja na njia mbadala ya kumpata daktari bingwa 'kimtandao'**



UKURASA 11

**MUFTI** aagiza dua maalum kwa Waislam nchini

UKURASA 3



**SHERIA** ya Uhujumu Uchumi kufanyiwa tathmini, kufumuliwa

UKURASA 3

# Walioshinda rufani wachapwa viboko

**Ni** kwa amri ya RC, aagiza walipe faini 300,000/- *UK. 2*



Jamii ya wafugaji kutoka Kijiji cha Magwailisi, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, wakijadiliana jambo juzi, kabla ya kuuzika mwili wa mmoja wa vijana watatu waliokutwa wameuawa na miili yao kutupwa katika Mto Ruaha Mkuu, kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wengine watatu wakiwa hawajulikani waliko. Picha ndogo: Mwili wa kijana huyo, ukiingizwa kaburini kwaajili ya maziko. Habari zaidi Uk. 16. PICHA: GRACE MWAKALINGA

## Daktari feki anaswa akidaiwa kutoa huduma za kibingwa

UKURASA 2

# Uchunguzi mauaji ya Blandina wakamilika

UK. 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** GOMES AUONA UBINGWA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Anaswa madai kutoa matibabu ya kibingwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKAZI wa Kijiji cha Mudio, Kata ya Romu wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, Othuman Kimaro, amekamatwa na vyombo vya dola akituhumiwa kujifanya daktari na kutoa huduma za kitabibu kwa wagonjwa, zikiwamo zinazotakiwa kutolewa na madaktari bingwa.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliagiza kukamatwa na kuhojiwa kwa Othuman baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuzuru kwenye zahanati bubu inayodaiwa kutumiwa na mtuhumiwa huyo kutibu wagonjwa, huku akiwa hana leseni ya kufanya kazi hiyo.

"Sasa hivi kuna mtoto yuko Hospitali ya Rufani ya KCMC amelazwa kule akipatiwa matibabu kwa sababu ya mambo haya. OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya) na Ofisa Mtendaji wa Kata hii. Huyu mtu ninawaachia hapa.

"Ahojiwe na aeleze kwa nini anahatarisha uhai wa watu? Anaweza kugharimu maisha ya watu hapa Mudio na kwingineko kwa kutoa huduma za tiba wakati hata serikali haimtambui.

"Anatoa dawa, anaandika rekodi za wagonjwa na anafanya kazi nyingine zinazostahili kufanywa katika ngazi ya vituo vya afya na hospitali za wilaya.

"Ana lundo la dawa hatari ambazo hazitakiwi kutolewa nje ya hospitali au vituo vya afya, ana vifaa na dawa za kuosha kizazi. Maana yake anaweza kuwa ndiye kinara wa kufanya abortion (kutoa mimba)," Ole Sabaya aliagiza.

Alipoulizwa na kiongozi huyo kuhusu shughuli zinazoendelea kwenye nyumba aliyokutwa yenye dawa na duka la dawa, mtuhumiwa huyo alidai anatoa huduma za kifedha zinazotolewa kupitia miamala ya mitandao ya simu.

Akizungumza baada ya ukaguzi kufanyika katika zahanati bubu iliyoko Mudio, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Irine Haule, alisema:

"Leo Aprili 28 (jana), tumekuja na Mkuu wa Wilaya katika Kijiji cha Mudio, kuna mtu ambaye alikuwa analalamikiwa na wananchi kutoa huduma za afya kinyume cha utaratibu.

"Kimsingi, huyu mtu yeye mwenyewe anadai kwamba ni mtaalamu wa afya lakini amestaafu. Mpaka sasa sijafanikiwa kuona vyeti vyake vya afya. Pia tumekuta duka lenye dawa nyingi za kunywa pamoja na za kuchoma.

"Lakini kuna vifaa vingi ambavyo vinatumika katika hospitali na vifaa vya kutolea huduma. Vimo vifaa vya kusafisha vizazi, sindano pamoja na dripu.

"Kwa hiyo kimsingi anachokifanya ni kosa. Huyu bwana (Othuman), serikali haimtambui lakini pia taratibu anazozitumia kutolea huduma ni taratibu ambazo hazijafuata misingi ya miongozo ya wizara kama zilivyowekwa.

"Tumeona ana hizo dawa na sindano lakini mazingira ambayo anatolea huduma siyo sahihi. Ukiangalia katika matumizi yake ya dawa, anafanya kuandika kwenye makaratasi na kwenda kwenye maduka makuwa kununua."

Kutokana na upungufu huo, Dk. Haule aliwataka wenye maduka makubwa ya dawa kuchunguza mtu anayepaswa kwenda kununua dawa nyingi, hasa dawa hatari kwamba ni vyema mtoa huduma, akawa na uthibitisho kama anayenunua ana kibali cha kupata hizo dawa.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Philip Mangula (kulia), akiongoza kikao maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM jijini Dodoma jana. Kutoka kulia ni Wajumbe; Rais mstaafu wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti Visiwani, Dk. Ali Mohamed Shein, Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. **PICHA: OMR**

# Walioshinda rufani wachapwa viboko

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameamuru wanafunzi saba kati ya 20 wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Iyunga jijini Mbeya waliokuwa wanatuhumiwa kuchoma moja ya majengo ya shule hiyo, kucharazwa bakora tano na kulipa Sh. 300,000 kila mmoja licha ya kushinda rufani zao.

Wanafunzi hao baada ya kufukuzwa shuleni Machi 18, mwaka huu, walikata rufani kwenye Kamati ya Rufani ya Mkoa ambayo iliridhiwa warejee shuleni.

Chalamila pia ameagiza shule hiyo kuwa chini ya ulinzi wa vyombo ambavyo hajaviweka wazi na kuagiza mwanafunzi yeyote atakayekamatwa nje ya shule muda ambao hauruhusiwi kisheria, akamatwe na kupelekwa 'selo'.

Vilevile, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wanafunzi wote wanaodaiwa kuvunja maduka na nyumba za walimu na kuiba ili wawajibishwe kwa mujibu wa sheria ili kukomesha vitendo hivyo.

Chalamila alitoa uamuzi huo jana alipoiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo kuitembelea shule hiyo kwa ajili ya kuangalia uharibifu uliofanywa na wanafunzi hao.

Kabla ya Chalamila kutoa uamuzi huo, Mkuu wa Shule hiyo, Edward Mwantimo, alibainisha kuwa baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakikiuka miiko na taratibu za shule ikiwamo kumiliki simu, kutoroka shuleni usiku na kwenda kuzurura mitaani. Alibainisha kuwa hivi karibuni walifanya msako na kukamata simu walizokuwa wanazitumia na wanafunzi hao na kisha wakaanza vikao vya kisheria vya shule ikiwamo kikao cha nidhamu kwa ajili ya kushughulikia tatizo hilo.

Mkuu wa Shule huyo aliendelea kubainisha kuwa wakati wanaendelea na vikao hivyo, baadhi ya wanafunzi walichoma stoo ya nidhamu lakini baada ya wenzao kushtuka, walipiga kelele na moto ukadhibitiwa haraka kwa ushirikiano kati ya wanafunzi na walimu.

Alisema wanafunzi hao wamekuwa wakichuna nyaya za umeme na kujiunganishia umeme kwa ajili ya kuchaji simu, hali ambayo imekuwa ikihatarisha majengo ya shule hiyo kuungua.

"Moto huo uliwashwa Machi 10, mwaka huu saa saba usiku na usingedhibitiwa mapema, ungeteketeza madarasa hayo nyuma, ya ofisi ya walimu na mabweni yote.

"Tulifanya jitihada za kuwabaini wahusika na ndipo tukawabaini vijana 20 ambao bodi ya shule iliamua kuwafukuza," Mwalimu Mwantimo alisema.

Kiongozi huyo wa shule alisema baadhi ya wanafunzi huwa wanatoroka nyakati za usiku na kwamba wakati mwingine huwa wanakamatwa na askari wanaokuwa kwenye oparesheni za usiku na wanapohojiwa huwa hawakiri kuwa ni wanafunzi mpaka wanapokuwa wamebanwa.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Majuto Njanga, alisema uamuzi wa kuwafukuza wanafunzi hao ulifanyika Machi 18, mwaka huu lakini saba kati yao, walikata rufani kwenye Bodi ya Rufani ya Mkoa ambayo Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Mkoa.

Alisema bodi hiyo iliridhia wanafunzi hao kurejeshwa shuleni kwa masharti ya kugharimia ukarabati wa chumba kilichounguzwa, kucharazwa bakora na kwa wale ambao ni wa madarasa ya mitihani, wamalizie masomo yao wakitokea nyumbani.

Njanga aliutaka uongozi wa shule hiyo kuwaondoa mapema wanafunzi wote wanaokiuka miiko na miongozo ya Wizara ya Elimu ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na tabia zao.

"Mwanafunzi ambaye anatoka nje ya shule ni lazima awe kwenye sare za shule vinginevyo hatufai, ni heri tukawa na wanafunzi wachache wenye nidhamu kuliko kuwa na wengi ambao mienendo yao ni mibovu.

Ninawaomba wanangu mjue kwamba elimu ndiyo mkombozi wenu, ulipewa maelekezo yako peke yako lakini unaweza ukaondoka hapa kwa kuiga makundi," alionya.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa Mkoa Chalamila aliwaamuru wanafunzi hao kupiga 'push up' na akaamuru mmoja wa walimu wa shule hiyo kuwacharaza bakora tano kila mmoja.

"Wa kidato cha nne na sita ambao watakuwa na mitihani hivi karibuni, watafanya mitihani wakitokea nyumbani na kila wanapomaliza mtihani mmoja, watatoka nje ya shule, tutaweka askari wawili getini kwa ajili ya kuwashughulikia watakapogoma kutoka," alisema Chalamila.

Alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, kushirikiana na Mkuu wa Shule hiyo kudhibiti tabia za wanafunzi hao ikiwamo kuwalaza selo na kuwacharaza bakora.

# Polisi yakamilisha uchunguzi mauaji ya Blandina

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kinondoni, limesema limekamilisha uchunguzi wa tuhuma za mauaji ya mwanahabari wa ITV/Redio One, Blandina Sembu na jalada la uchunguzi huo limekabidhiwa kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Ramadhani Kingai, aliiambia Nipashe jana kwa njia ya simu kuwa hadi sasa wanaendelea kumshikilia mtuhumiwa mmoja ambaye ni dereva wa bodaboda, huku wakimsubiri DPP kwa hatua zaidi. Hata hivyo, hakufafanua zaidi.

Wiki chache zilizopita, jeshi hilo lilisema linamshikilia dereva bodaboda kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya mwanahabari huyo.

Blandina ambaye pia alikuwa mtayarishaji wa kipindi cha Jarida la Wanawake ITV, alikutwa akiwa amefariki dunia Machi 27, mwaka huu, baada ya mwili wake kukutwa umetupwa katikati ya barabara ya Bamaga-ITV, Mwenge, jijini Dar es Salaam.

Uchunguzi wa awali wa polisi, ulibaini kuwa kifo cha Blandina kilisababishwa na kupigwa na kitu chenye ncha kali usoni.

Kamanda Kingai alisema mwili wa Blandina ulikutwa umetelekezwa eneo la baa ya Maryland, njia panda ya kituo cha ITV, baada ya watu wasiofahamika wakiwa na gari aina ya Noah, ambalo halikutambuliwa namba yake ya usajili, kuutelekeza mwili huo.

"Walisimamisha gari eneo hilo kwa muda mfupi na lilipoondoka ulipatikana mwili wa jinsia ya kike, alitambulika kuwa ni Blandina Sembu (47), mfanyakazi wa ITV, Redio One," alisema Kamanda Kingai.

Kamanda huyo alisema kuwa, Blandina alikuwa ni mkazi wa Zinga, Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Mwili wa Blandina uliagwa jijini Dar es Salaam, Machi 31, mwaka huu na kisha kusafirishwa kwa maziko Musoma, mkoani Mara.

## HABARI KITAIFA

# Sheria uhujumu uchumi kufanyiwa tathmini

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imeanza kuzifanyia tathmini sheria sita ikiwamo Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, imeelezwa.

Lengo kuu la kufanya hivyo ni kubainisha endapo zinaweza kutumika kupunguza msongamano wa mahabusi magerezani na kupunguza gharama za uendeshaji magereza.

Zingine ni Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291; Sheria ya Bodi ya Msamaha, Sura ya 400 na Sheria ya Kikomo cha Adhabu, Sura ya 90.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema hayo jana wakati akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2021/22.

"Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inaandaa taarifa mbili za tathmini ya utekelezaji wa sheria zinazohusu mifumo ya kutoa adhabu mbadala na uboreshaji wa Sekta ya Utalii".

"Katika mfumo wa sheria za adhabu mbadala, sheria zinazofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200; Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291; Sheria ya Bodi ya Msamaha Sura ya 400 na Sheria ya Kikomo cha Adhabu, Sura ya 90," alisema.

Kuhusu uboreshaji wa sekta ya utalii, Profesa Kabudi alisema sheria zinazofanyiwa tathimini ni pamoja na Sheria ya Utalii Sura ya 65; Sheria ya Wanyamapori Sura ya 283; Sheria ya Mbuga za Wanyama Sura ya 282; Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura ya 281; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Mamlaka ya Ngorongoro Sura ya 284; na Sheria ya Malikale Sura ya 333.

Alisema tathmini katika sekta ya utalii inalenga kubaini endapo sheria zilizopo zinaweza kutumika kuongeza makusanyo ya mapato na utunzaji endelevu wa vivutio vya utalii.

Prof. Kabudi pia alisema wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza makubaliano ya kumaliza kesi za jinai chini ya utaratibu wa washitakiwa kukiri makosa yao (plea bargaining) kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 11 ya Mwaka 2019.

Alisema katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, mwaka huu, kesi 192 zilihitimishwa kwa njia hiyo na washitakiwa 243 walikiri makosa na kulipa serikalini Sh. bilioni 35.073 kama fidia kwa serikali pamoja na faini kutokana na makosa ya uhujumu uchumi.

Waziri alisema jambo hilo ni endelevu na fedha hizo zimewekwa katika akaunti maalum iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kadhalika, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi za jinai, walipewa adhabu mbalimbali zikiwamo za vifungo, faini na mali kutaifishwa.

Alisema Sh. bilioni 1. 230 zililipwa mahakamani kwa ajili ya faini katika kesi 4,738. Katika kipindi hicho, pia mali mbalimbali zilitaifishwa kuwa mali ya serikali.

Prof. Kabudi alizitaja mali hizo ni pamoja na fedha taslimu Sh. bilioni 5.554, magari 14, nyumba tatu, pikipiki sita, magogo 105, mbao 3,205, seti moja ya kompyuta, kompyuta mpakato mbili, runinga mbili, kamera moja, meno ya tembo mawili, meno ya kiboko matatu na madini ya almas karats 71,654 yenye thamani ya Dola za Marekani 29,509,821.84.

Pia alisema wizara kupitia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa na mashauri ya madai ya kimataifa 20, kati ya hayo, mashauri manne yamemalizika na 16 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Alisema katika kuendesha mashauri hayo ya madai ya kitaifa na kimataifa, serikali imeokoa kiasi cha Sh. bilioni 132.245 ambacho kingelipwa kwa wadai endapo serikali ingeshindwa kesi hizo.

# Mufti awataka Waislamu kuliombea taifa

**Na Christina Haule,** MOROGORO



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Bin Zubeir.

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeanzisha kanzidata ya madhira yanayowapata wanahabari yatakayosaidia kuongeza nguvu ya ushahidi wakati wa kesi mbalimbali za kuzuia Uhuru wa wanahabari.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya uhuru wa habari na haki ya kupata taarifa kwa waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali yaliyoandaliwa na baraza hilo yanayofanyika mjini hapa.

Alisema kuna wanahabari wamekuwa wakipigwa na kunyimwa uhuru wao wa kupata taarifa na pengine kuvunjiwa vifaa vyao vya kazi jambo ambalo si sahihi kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

Ukusanyaji kanzidata hiyo, alisema utasaidia kuongeza ushawishi na utetezi kwa wanahabari wanapokumbwa na madhira na kwamba ikiwa itasema sheria ina upungufu mbalimbali, inabidi kuwe na ushahidi.

Mukajanga alisema kupatikana kwa data zinazohusiana na upatikanaji wa taarifa kutaleta njia rahisi ya haki ya kupata taarifa kwa wanahabari wakati wanapofanya ushawishi na uzengezi.

Naye Mratibu kutoka MCT, Saumu Mwalimu, aliitaka jamii kutambua kuwa kila mtu anahaki ya kupata taarifa na kwamba wapo wananchi wengi bado hawajajua hilo.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 778 | 1,758 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,823 | 13,599 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 48,793 | 49,837 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 977 | 3,549 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 19,846 | 18,803 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 72,504 | 69,749 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,024 | 2,608 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,081 | 1,947 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **162,826** | **161,850** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 53,146 | 53,125 |
| 18 | Amana za Wateja | 69,231 | 68,384 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 89 | 28 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,340 | 2,772 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,477 | 1,526 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **126,308** | **125,859** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **36,518** | **35,991** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,570 | 2,479 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 11,908 | 10,974 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 540 | 1,037 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **36,518** | **35,991** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 8,764 | 10,751 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,609 | 2,600 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 220 | 195 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.43% | 22.24% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.59% | 3.72% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 59.43% | 57.56% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 44.53% | 43.09% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.82% | 85.62% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.71% | -3.53% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.60% | -2.91% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 3,074 | 3,108 | 3,074 | 3,108 |
| 2 Gharama za Riba | 1,230 | 1,272 | 1,230 | 1,272 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,844** | **1,836** | **1,844** | **1,836** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 25 | 303 | 25 | 303 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **116** | **173** | **116** | **173** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 40 | 58 | 40 | 58 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 76 | 115 | 76 | 115 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,176** | **1,163** | **1,176** | **1,163** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 487 | 430 | 487 | 430 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 689 | 733 | 689 | 733 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **759** | **543** | **759** | **543** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 219 | 269 | 219 | 269 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **540** | **274** | **540** | **274** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **540** | **274** | **540** | **274** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 30 | 29 | 30 | 29 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 100 | 51 | 100 | 51 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.87% | 1.43% | 1.87% | 1.43% |
| (ii) Wanahisa | 5.81% | 3.08% | 5.81% | 3.08% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 36.87% | 35.45% | 36.87% | 35.45% |
| (iv) Zinazozalisha | 5.32% | 5.58% | 5.32% | 5.58% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.01.2021** | **21,500** | - | **12,012** | **2,479** | - | - | **35,991** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 540 | - | - | - | **540** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (92) | 92 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | (13) | | | | **(13)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.03.2021** | **21,500** | - | **12,447** | **2,571** | - | - | **36,518** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.10.2020** | **21,500** | - | **11,442** | **3,328** | - | - | **36,271** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (203) | - | - | - | **(203)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 849 | (849) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (76) | - | - | - | **(76)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.12.2020** | **21,500** | - | **12,012** | **2,479** | - | - | **35,991** |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 759 | (375) | 759 | 543 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 208 | 1,049 | 208 | 342 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (961) | 2,172 | (961) | (3,745) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 868 | (4,452) | 868 | 5,488 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 1,069 | 5,031 | 1,069 | 1,145 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (421) | 276 | (421) | (687) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,032 | (1,923) | 2,032 | 3,355 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (219) | 127 | (219) | (269) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***3,335*** | ***1,904*** | ***3,335*** | ***6,172*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (3) | (66) | (3) | (5) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(3)*** | ***(66)*** | ***(3)*** | ***(5)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (387) | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | ***(387)*** | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **3,332** | **1,451** | **3,332** | **6,167** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 32,540 | 31,089 | 32,540 | 23,432 |
| | **Robo Mwaka** | **35,872** | **32,540** | **35,872** | **29,599** |

BOI (TANZANIA) LTD
DAR ES SALAAM

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mkuu | | 27.04.2021 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>Mkuu wa Fedha | | 27.04.2021 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | 27.04.2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi | | 27.04.2021 |
| 2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi | | 27.04.2021 |

# Mbatia: Utashi wa kisiasa muhimu kwa maendeleo

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amesema ili kurejesha nchi katika demokrasia, haki na uhuru wa kujieleza, kunahitajika utashi wa kisiasa.

Amesema vyama vya upinzani havifanyi vizuri katika nyanja ya kisiasa hali inayosababisha kuwapo kwa hoja dhaifu ambazo hazina mustakabali mzuri kwa taifa.

Katika mahojiano maalumu na Nipashe, Mbatia amezungumzia masuala mbalimbali, ikiwamo hali ya kisiasa, demokrasia, haki na uhuru wa kujieleza.

**Swali: Unaonaje hali ya kisiasa hivi sasa nchini?**

**Jibu:** Ninaweza kusema hivi, hali ya kisiasa nchini ipo kwa namna hii, ila kwanza umma ufahamu maana ya siasa. Siasa kwa wanaoamini kwamba Mungu yupo, kwenye mambo ya uumbaji, ni kwamba kila binadamu ana fikra tofauti na mwenzake na ni haki ya msingi. Unaweza ukakubali kwamba ukifikiri sana ikafikia hatua kwamba imani za dini, sayansi, siasa vimekuwa kitu kimoja.

Mwaka 1633 Kanisa Katoliki lilimpinga mtu aliyesema dunia inazunguka jua, huyu alikuwa Galileo Galilei, ambaye alihukumiwa kufungwa, kwa kauli hii. Baadaye mwaka 1992, Papa Yohane Paulo II, aliomba radhi kuwa hiyo hukumu haikuwa sahihi.

Kwa kuwa sisi ni binadamu na tuna mawazo tofauti kila mmoja atasema twende Kaskazini, Kusini mwingine Magharibi, Mashariki, ili kuafikiana tufanye lipi lazima fikra ziwe pamoja kwa kukubaliana twende upande huu, ili kuifanya dunia iwe sehemu salama ya kuishi.

Katika muktadha huo, siasa ndio huileta jamii pamoja na kukubaliana itikadi yetu, imani iwe namna gani ili tuishi. Kila mmoja anaonesha ushawishi wa itikadi yake utakuwaje, ili kutofutisha chama kimoja na kingine.

**Swali: Nini umuhimu wa vyama vya upinzani kisiasa?**

**Jibu:** Vyama vya siasa vipo kwa ajili ya kushindanisha hoja. Na ili kuifanya Tanzania kuwa sehemu nzuri ya kuishi kuna utaratibu wa kikatiba. Utaratibu huu ili ufanyike kuna Katiba iliyoweka misingi. Katiba ya sasa ya mwaka 1977, inatoa nafasi, haki ya chama cha siasa kufanya kazi kwa misingi iliyowekwa.

Kuna kanuni, sheria, ili kujumuika pamoja, kufanya mikutano ya hadhara kwa vyama, ni haki ya kimsingi.

Pamoja na mabadiliko yote yaliyofanyika katika Katiba hii bado ni ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, itikadi imeandikwa kwenye Katiba kuwa ni ya ujamaa na kujitegemea.

Ibara ya 10 inasema CCM itakuwa ni chama pekee, ikafutwa. Ilivyofutwa na nyingine zikabaki kama ilivyo, hii ikatupa shida, japo ibara moja inatoa haki, nyingine inafinyanga hiyo haki.

Wanazuoni walisema Katiba itokane na umma. Kwa hiyo Katiba hii inatoa haki na wakati huohuo ina upungufu mwingi.

Mwaka 1991 tuliweka msukumo wa kuandikwa kwa Katiba Mpya na kuingia mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Tulikutana kwa siku mbili na kuanzisha Kamati ya Jaji Nyalali, kuliza Watanzania inatakiwa Katiba ipi. Lakini waliokuwa madarakani hawakutaka kutekeleza yaliyokuwa kwenye Tume, zaidi walibeba pendekezo la kuwa na vyama vingi.

Mfumo mwingine ukabaki kama ulivyo, vyama vingi vipo lakini kwa hisani ya chama kimoja.

Chama cha Mapinduzi kilisajiliwa moja kwa moja bila utaratibu kwa kuomba kama chama cha siasa, ndio maana kuna hoja nyingi za msingi kuwa CCM sio chama cha siasa bali ni chama dola kwa mujibu wa sheria.

Baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa ilitakiwa vyama vianze kusajiliwa. Sheria mpya ikasema CCM ilisajiliwa moja kwa moja bila utaratibu wa kupata wanachama 200 katika mikoa ikiwamo Zanzibar.

**Swali: Kwa nini kuna ukimya wa kisiasa kwa vyama vya siasa, hasa upinzani?**

**Jibu:** Hamu kubwa kwa wananchi ni kuwa na kitu kinachoitwa utashi wa kisiasa. Mambo yanayohusu siasa kuzingatiwa kwa upana wake.

Vyama vinatakiwa kufanya majukumu yake kwa kushindana, lakini vikisimamiwa na chama kilichopo madarakani, chama dola, ambacho tangu uhuru ni kilekile, tunasema ni chama dola sababu kinachukua muundo wa serikali. Vyombo vyote ikiwamo vya ulinzi na usalama vinaripotiwa kwake kwa chama kilichopo madarakani.

Kwenye hali ya namna hiyo hivi sasa ushindani wa fikra, hamasa za maendeleo endelevu kunadumazwa na siasa kwa kutokuwapo uwanja sawa wa siasa.

Utaratibu ukiwa si hai, unadumaza siasa. Sasa hivi kuna kasi ya kutaka mfumo wa vyama hivi ni hoja kielelezo. Ukiangalia mtawanyo wa umri wa watu wazima, wenye umri wa miaka 16 hadi 54 ni asilimia 85 ya Watanzania wote. Hawa wote wamezaliwa baada ya Muungano.

Kuna hoja zinazoibuka kutoka kwa wananchi ambazo zinakosa uendelevu, ni kiburi cha wanasiasa kujiona bora kuliko mwingine. Sisi wanasiasa tunaoleta kiburi cha kisiasa kwenye jamii.

Swali: NCCR-Mageuzi inaendeleaje katika ulingo wa kisiasa kwa kutofanya mikutano?

Jibu: Kwenye Katiba vyama vinaruhusiwa mikutano, ninaweza kusema kipindi hiki serikali haikuwa rafiki wa demokrasia, Tanzania tunaihitaji zaidi dunia, kuliko sisi tunavyoihitaji.

Huwezi ukazungumzia jambo lolote kabla ya kuzungumzia haya manne, utawala wa sheria, utawala bora, demokrasia na haki za binadamu. Ukitaka kuzungumza jambo lolote ikawa hakuna nafasi. Ustawi wa mwanadamu kulinda uhai wake, kifikra, mawazo mbadala.

Maendeleo ni watu si vitu. Ubunifu wa Mwalimu Nyerere kuunganisha watu kuzungumza lugha moja ya Kiswahili, ni maendeleo.

**Swali: Vyama vya siasa vimeathirika vipi?**

**Jibu:** Sio tu imeathiri vyama vya siasa, imerudisha nyuma Tanzania kwenye ujima. Hii imeturudisha Watanzania kuzungumza hoja zisizo na msingi kwenye maofisi, vyama vyetu hasa kuhusu ukabila, vyama tumerudi kuzungumzia udini, maeneo, kila mtu kumtilia shaka mwenzake. Marufuku hii imeathiri na kudhoofisha upinzani na hata CCM yenyewe. Itachukua miaka takribani 10, kurudi tena.

Tanzania imeshika nafasi ya 153 kati 156 ya watu wake kuwa na furaha. Hii ni kurudi nyuma kwa maendeleo ya kifikra, demokrasia. Uhuru wa taarifa, kushirikishana ni muhimu sana.

**Swali: Unazungumziaje serikali awamu ya sita?**

**Jibu:** Tunahitaji meza ya majadiliano tukijadiliana katika meza ya mazungumzo, tutajua tufanye nini. Ukiniuliza kwenye hiyo meza cha kwanza tutengeneze tume ya majadiliano kuleta suluhu na maridhiano kwa mambo ya msingi.

Hapo itapatikana, Tume Huru ya Uchaguzi, Katiba Mpya, meza ya majadiliano itazaa maafikiano. Rais atakuwa amejijengea heshima kwa kuundwa kwa tume ya suluhu, na kisha twende kwenye Katiba.

Mimi nitasema kuhusu Katiba, nitasema twende na ya Jaji Warioba, au tuamue kufanya mabadiliko katika Katiba hii ya mwaka 1977 iliyopo, tutakubaliana.

Ili kuzaa mwafaka wa kitaifa tunaweza kujifunza kutoka hata Zanzibar, aliifanya Maalim Seif (marehemu), Kenya walifanya na tulishiriki katika meza ya mazungumzo.

Mwaka 2013, watu 96 akiwamo rais, maspika, makamu wa rais, viongozi wa dini na serilaki, tulikaa kwa siku chache tulimaliza hali ambayo kipindi hicho ilihatarisha usalama na amani.

Ili mama (Rais Samia) aweze kufanikiwa utashi kisiasa uwepo.

**Swali: Nini kifanyike kufikia Tanzania ya maendeleo na demokrasia?**

**Jibu:** Katiba inazungumzia yote, Tume ya Uchaguzi ipo kwenye Katiba, Msajili wa vyama yumo katika Katiba, ukiwa na Katiba Mpya kila kitu kitazaliwa kipya.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa itafanya kazi yake. Mfano tangu vyama vilipopigwa marufuku hakuna hata chama kimoja kilichosajiliwa, uhuru wa mahakama vyote vitapatikana kupitia Katiba.

**Swali: Ukikutana na Rais Samia ukiwa Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, una ajenda gani za kumpa?**

**Jibu:** Hivi karibuni Kamati Kuu ya chama ilipokutana siku mbili, tulizungumza mambo mengi na Machi 29, mwaka huu, tulimuandikia barua Rais Samia, kumpongeza, tulimwambia tupo tayari kufanya naye kazi katika kustawisha mifumo yenye kujali utu wa mwanadamu.

Alitujibu April 14, mwaka huu, na tunasubiri akituita tuzungumze masuala ya msingi, kama chama upande wetu, Katiba, lakini kuu la msingi ni kuhusu mifumo imara ambayo huzaa haki na amani.

**Swali: Vyama vya upinzani ni kundi lenye tafsiri gani kwenye jamii?**

**Jibu:** Mfano kuna wabunge ambao wamekataliwa na vyama vyao, lakini mhimili wa Bunge unasema hapana tunawatambua hawa ni wabunge. Kuna fujo zinatokea kwenye siasa na kupunguza au kuondoa imani.

Fujo kwenye vyama inatokana na imani kushuka na kutoaminiana. Hakuna utaratibu wa kutekelezeka kama ilivyowekwa.



Mwenyekiti wa chama cha NCCR-Mageuzi Taifa, James Mbatia akisisitiza jambo, wakati wa mahojiano na gazeti hili, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TANGAZO

# TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

NMB Karibu yako

Trilioni **4.3** Mikopo Halisi Iliyopo **+11%** YoY

Trilioni **5.3** Amana za Wateja **+9%** YoY

Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi **5%**

Mapato Bilioni **224** **+16%** YoY

Faida kabla ya Kodi ya Mapato Bilioni **93** **+34%** YoY

Faida Baada ya Kodi ya Mapato Bilioni **65** **+33%** YoY

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **48%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31 03.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31 12.2020 | Robo Mwaka ya sasa 31 03.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31 12.2020 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 470,009 | 661,689 | 470,009 | 661,689 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 529,551 | 385,799 | 529,551 | 385,799 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,207,987 | 1,304,253 | 1,207,987 | 1,304,253 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 142,592 | 130,925 | 142,592 | 130,925 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3,956 | 1,449 | 3,956 | 1,449 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 2,384 | - | 2,384 | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 46,514 | 39,904 | 46,514 | 39,904 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,130,048 | 4,108,789 | 4,130,448 | 4,109,260 |
| 12 | Mali Nyingine | 200,389 | 206,893 | 274,379 | 280,336 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 207,893 | 215,715 | 174,232 | 181,562 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **6,944,243** | **7,058,336** | **6,984,972** | **7,098,097** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 57,131 | 131,224 | 57,131 | 131,224 |
| 18 | Amana za Wateja | 5,188,989 | 5,247,973 | 5,192,578 | 5,247,978 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 30,874 | 36,645 | 30,874 | 36,645 |
| 20 | Amana Maalumu | 6,301 | 40,833 | 6,301 | 40,833 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,121 | 2,118 | 2,121 | 2,118 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 57,879 | 36,682 | 57,723 | 36,683 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 37,470 | 36,831 | 37,470 | 36,831 |
| 27 | Dhima Nyingine | 64,660 | 71,146 | 103,870 | 112,112 |
| 28 | Madeni | 302,620 | 323,740 | 302,620 | 323,740 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **5,748,045** | **5,927,191** | **5,790,688** | **5,968,163** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,196,198** | **1,131,145** | **1,194,284** | **1,129,934** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,106,441 | 896,141 | 1,109,142 | 903,340 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 65,387 | 210,300 | 64,684 | 205,802 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 458 | 792 | 458 | 792 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,912 | 3,912 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,196,198** | **1,131,145** | **1,194,284** | **1,129,934** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 654,587 | 624,881 | 654,587 | 624,881 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 216,506 | 231,287 | 216,506 | 231,287 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 209,527 | 204,809 | 209,527 | 204,809 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 9,058 | 10,055 | 9,058 | 10,055 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 17% | 16% | 17% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5% | 5% | 5% | 5% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82% | 78% | 82% | 78% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 59% | 58% | 59% | 58% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79% | 79% | 79% | 79% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -3% | 3% | -3% | 3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -2% | 2% | -2% | 1% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 31.03.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 | Robo ya Mwaka sasa 31.03.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.03.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.03.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 190,769 | 166,022 | 190,769 | 166,153 | 190,769 | 166,022 | 190,769 | 166,153 |
| 2 | Gharama za Riba | (32,859) | (32,597) | (32,859) | (32,597) | (32,859) | (32,597) | (32,859) | (32,597) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **157,910** | **133,425** | **157,910** | **133,556** | **157,910** | **133,425** | **157,910** | **133,556** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (22,870) | (21,847) | (22,870) | (21,847) | (22,870) | (21,847) | (22,870) | (21,847) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **65,687** | **59,773** | **65,687** | **59,773** | **65,687** | **59,773** | **65,687** | **59,773** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 5,574 | 5,817 | 5,574 | 5,817 | 5,574 | 5,817 | 5,574 | 5,817 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 55,821 | 50,171 | 55,821 | 50,171 | 55,821 | 50,171 | 55,821 | 50,171 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 4,292 | 3,785 | 4,292 | 3,785 | 4,292 | 3,785 | 4,292 | 3,785 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(107,034)** | **(100,458)** | **(107,737)** | **(101,881)** | **(107,034)** | **(100,458)** | **(107,737)** | **(101,881)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (56,463) | (50,517) | (56,463) | (50,517) | (56,463) | (50,517) | (56,463) | (50,517) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (3,548) | (2,479) | (3,548) | (2,479) | (3,548) | (2,479) | (3,548) | (2,479) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (47,023) | (47,462) | (47,726) | (48,885) | (47,023) | (47,462) | (47,726) | (48,885) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **93,693** | **70,892** | **92,990** | **69,601** | **93,693** | **70,892** | **92,990** | **69,601** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (28,306) | (20,880) | (28,306) | (20,880) | (28,306) | (20,880) | (28,306) | (20,880) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **65,387** | **50,012** | **64,684** | **48,721** | **65,387** | **50,012** | **64,684** | **48,721** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **(334)** | **23** | **(334)** | **23** | **(334)** | **23** | **(334)** | **23** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **65,053** | **50,035** | **64,350** | **48,744** | **65,053** | **50,035** | **64,350** | **48,744** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,474 | 3,450 | 3,474 | 3,450 | 3,474 | 3,450 | 3,474 | 3,450 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 131 | 100 | 129 | 97 | 131 | 100 | 129 | 97 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 4% | 3% | 4% | 3% | 4% | 3% | 4% | 3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 22% | 20% | 22% | 19% | 22% | 20% | 22% | 19% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 48% | 52% | 48% | 53% | 48% | 52% | 48% | 53% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11% | 11% | 11% | 11% | 11% | 11% | 11% | 11% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 31.03.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.12.2020 | Robo Mwaka ya sasa 31.03.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.03.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.03.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.03.2020 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 93,693 | 85,687 | 92,990 | 87,833 | 93,693 | 70,892 | 92,990 | 69,601 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 9,869 | 10,309 | 9,377 | 9,816 | 9,869 | 10,668 | 9,377 | 10,176 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (67,773) | (150,569) | (67,702) | (148,843) | (67,773) | (114,124) | (67,702) | (112,803) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (173,379) | 159,753 | (169,795) | 158,265 | (173,379) | (97,250) | (169,795) | (98,682) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (36,762) | 23,672 | (38,675) | (63,874) | (36,762) | (3,254) | (38,675) | (8,138) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3,728 | 16,478 | 3,181 | 102,133 | 3,728 | 25,951 | 3,181 | 32,729 |
| - Kodi Iliyolipwa | (26,436) | (35,006) | (26,436) | (35,006) | (26,436) | (19,021) | (26,436) | (19,021) |
| - Mengineyo (bainisha) | 9,296 | 10,472 | 9,296 | 10,472 | 9,296 | 12,630 | 9,296 | 12,630 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(187,764)** | **120,796** | **(187,764)** | **120,796** | **(187,764)** | **(113,508)** | **(187,764)** | **(113,508)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (3,919) | (8,272) | (3,919) | (8,272) | (3,919) | (4,361) | (3,919) | (4,361) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | 95,934 | (121,915) | 95,934 | (121,915) | 95,934 | (168,983) | 95,934 | (168,983) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **92,015** | **(130,187)** | **92,015** | **(130,187)** | **92,015** | **(173,344)** | **92,015** | **(173,344)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (21,120) | (22,225) | (21,120) | (22,225) | (21,120) | (26,274) | (21,120) | (26,274) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(21,120)** | **(22,225)** | **(21,120)** | **(22,225)** | **(21,120)** | **(26,274)** | **(21,120)** | **(26,274)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(116,869)** | **(31,616)** | **(116,869)** | **(31,616)** | **(116,869)** | **(313,126)** | **(116,869)** | **(313,126)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 907,029 | 938,645 | 907,029 | 938,645 | 907,029 | 1,213,370 | 907,029 | 1,213,370 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **790,160** | **907,029** | **790,160** | **907,029** | **790,160** | **900,244** | **790,160** | **900,244** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,106,441** | - | - | **4,704** | **1,131,145** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 65,387 | - | - | - | 65,387 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (334) | (334) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,171,828** | - | - | **4,370** | **1,196,198** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **944,472** | - | - | **4,630** | **969,102** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 50,012 | - | - | - | 50,012 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 23 | 23 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **994,484** | - | - | **4,653** | **1,019,137** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,109,142** | - | - | **792** | **1,129,934** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 64,684 | - | - | - | 64,684 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (334) | (334) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,173,826** | - | - | **458** | **1,194,284** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **951,340** | - | - | **1,049** | **972,389** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 48,721 | - | - | - | 48,721 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 23 | 23 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,000,061** | - | - | **1,072** | **1,021,133** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA MACHI 2021

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Afisa Mtendaji Mkuu** | | Aprili 21, 2021 |
| Juma Kimori<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | | Aprili 21, 2021 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Aprili 21, 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na PricewaterhouseCoopers, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | | Aprili 21, 2021 |
| Leonard Mususa<br>**Mkurugenzi** | | Aprili 21, 2021 |

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utatuzi wa kero hii Muungano ni fursa, kilichobaki utaratibu

**BUNGE** juzi lilielezwa kuwa kero tano za Muungano zimepata ufumbuzi wa kudumu, na kubwa ni kodi kwenye baadhi ya bidhaa kutoka Visiwani Zanzibar, kuja Tanzania Bara.

Kauli ya serikali juu ya suala hilo ni neema na fursa kubwa kwa Watanzania wa pande zote za Muungano; kwamba sasa mtu anaweza kununua gari au bidhaa nyingine akaingia nayo Bara bila kikwazo cha kutozwa kodi mara mbili.

Kwa muda mrefu kumekuwa na kilio cha wananchi kwamba anaponunua gari visiwani humo, sukari au TV ambazo kule ni bei nafuu kuliko Bara anapofika bandarini anakutana na watu wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), ambao hutoza kodi kama bidhaa iliyotoka nje ya nchi.

Tunaipongeza serikali kwa kuhakikisha kero hii kati ya kero 25 inatatuliwa, na Jumatatu Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, katika sherehe za Muungano alieleza kuwa kero 15 zimeshatatuliwa, na tunaamini itapunguza ukali wa maisha kwa pande zote.

Kwa kero hii kupatiwa ufumbuzi, maana yake kasi ya bidhaa kuingia nchini itaongezeka, lakini ni muhimu kukawa na tahadhari kubwa ili bidhaa za Bara zikakosa biashara kwa kuwa watu watakwenda Visiwani kununua bidhaa kwa bei ndogo.

Mathalani, bei ya sukari Visiwani ni Sh. 1,900 huku Bara ni Sh. 2,800 na jitihada za kushusha hadi Sh. 2,500 imeshindikana. Aidha, ushuru wa magari na vifaa vya umeme ulitozwa Zanzibar na Bara, hivyo kukwamisha wengi kufikisha bidhaa zao kwa ajili ya matumizi.

Angalizo linalotakiwa ni kuhakikisha suala la kodi ya ushuru wa forodha linakuwa na usawa ili kuepusha upande mmoja kuwa na bidhaa bei rahisi na kuwafanya watu kukimbilia huko kununua na zinazouzwa nchini zikadumaa.

Ni habari njema ambayo ni lazima itekelezwe kwa uangalifu kwa kuwa hakuna ubishi kuwa miaka ya nyuma wengi walikuwa wanakwenda Visiwani kununua bidhaa hizo kwa bei rahisi na kuja kuziuza Bara.


Bila kuwa na utaratibu mzuri maana yake kasi ya kuingiza bidhaa itaongezeka, lakini ni neema kubwa kwa kuwa sasa kasi ya biashara kati ya pande zote itaongezeka na kuimarika kwa maendeleo ya watu na taifa.

Ni muhimu sasa serikali zote mbili zikahakikisha kodi za pande zote ni rafiki kwa kuwa ni nchi moja. Kama kodi ya kuingiza gari Visiwani ni rahisi basi ni muhimu na Bara ikawa hivyo ili kuepuka kila mtu kukimbilia huko kuagiza gari ili kupunguza gharama.

Na iwapo kodi itakuwa ndogo kwa upande wa Visiwani maana yake itaua Bandari ya Dar es Salaam na nyingine ambazo ni maarufu kwa kupokea shehena ya magari kutoka nchi ya ng'ambo, na ndiyo muhimu wa kuwa na kodi sawa unapokuja.

Tunatarajia wananchi wote watatumia kwa uaminifu fursa zilizopatikana pande zote, na pia tunaamini serikali itaweka utaratibu mzuri ambao utakuwa ni wenye manufaa kwa wananchi wengi zaidi, huku ikikusanya kodi ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Sote tufungamane kufanikisha maudhui Wiki ya Chanjo, kugusa wengi kimaisha

Na Mary Geofrey

**WAKATI** Afrika inaadhimisha Wiki ya Chanjo, Tanzania, tunajivunia kutokomeza magonjwa kama ya donda koo, kifaduro, polio, pepopunda na surua.

Mengine katika orodha ni kifua kikuu, rubella, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, nimonia/kichomi, kuhara na saratani ya mlango wa kizazi.

Maadhimisho hayo yanafanyika kuanzia Aprili 24 hadi kesho na kaulimbiu ya mwaka huu duniani kote inatamka "Jamii iliyokingwa, Jamii yenye Afya Bora."

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wiki hii alifungua maadhimisho hayo kitaifa, kwenye viwanja vya Chamwino mjini Morogoro.

Dk. Gwajima anasisitiza madhumuni ya wiki hii, kwamba ni kuhamasisha na kuelimisha jamii umuhimu wa huduma za chanjo, kujikinga na magonjwa yanayozuilika na kujiepusha na vinavyozuilika, kwa chanjo.

Anaongeza, chanjo ni mkakati mwafaka kwa ama kutokomeza magonjwa au kupunguza vifo, hususani vya watoto wa umri chini ya miaka mitano na inapunguza gharama ambazo familia na taifa kwa jumla, zingetumia katika kutibu maradhi.

Waziri anataja takwimu kwamba chanjo, inazuia vifo kati ya milioni mbili hadi tatu kila mwaka, kwa maradhi yanayozuilika na chanjo duniani.

"Hapa nchini, mafanikio ya chanjo tumeyaona kwa kutokomeza magonjwa kadhaa ukiwamo wa surua ambao sasa tumefunga wodi zote za wagonjwa," alifafanua Dk. Gwajima.

Aidha, anataja kwamba miaka mitano illyopita, utoaji chanjo kitaifa ulikuwa asilimia 95, hali inayoikweza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri duniani katika chanjo.

Hadi sasa Tanzania imekwea kufikia Lengo Namba Nne la Malengo ya Milenia (SDG 4), kwa kupunguza vifo vya watoto chini ya umri miaka mitano kwa theluthi mbili, ambayo ni sawa na wastani asilimia 66.

Dk. Gwajima anasisitiza kwamba, kila mwananchi ana wajibu wa kuhakikisha mtoto au wa jirani asiyepata au kukamilisha chanjo, anapatiwa kulingana na ratiba yake, ikimwokoa kutoka hatari kwa afya yake na jamii inayomzunguka.

Waziri wa Afya, pia anaagiza vituo vyote vya kuduma afya, ambavyo havijaanza kutoa huduma za afya nchini, vianze mara moja kwa mama na mtoto, ili kupunguza vikwazo vya afya.

Mtazamo mkuu ni kwamba, kuanza kutoa huduma za mama na mtoto kwenye vituo vyote vya huduma za afya, kutasaidia kupunguzia mwendo mrefu kwa wajawazito na watoto wahitaji wa chanjo.

Katika hilo, Shirika la Afya Duniani (WHO) linatilia mkazo kuwafikia wananchi wanaokosa huduma hizo za chanjo nchini, ili kufikia hatua pale inapowezekana wayamalize kabisa magonjwa hayo kadrio inavyoowezekana, kupitia chanjo.

Mtaalamu wa Chanjo wa WHO nchini, Willium Mwengee, anasisitiza kukosekana chanjo kwa magonjwa makubwa yanayozuilika, inahatarisha magonjwa yanayolea pia, athari za umasikini, ulemavu, hata vifo nchini.

Anasema, ili kufanikisha hilo, WHO imeweka mwongozo unaohimiza mtu asitembee zaidi ya kilometa tano kufuata huduma za chanjo.

Katika hilo, jamjii pia ina wajibu wa kuhakikisha watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanapatiwa chanjo, ili kuwakinga na maradhi hayo tajwa.

Hapi ndipo kunapozaa wajibu wa wazazi kufuata sheria na kanuni zote za afya zinazotolewa na WHO na za kitaifa, kwa kufuata ratiba zilizowekwa.

Wanajamii nao wanapaswa kujiepusha na yasiyo sahihi, kama vile maneno potofu na imani za kishirikina kuhusu chanjo, huku ikifahamika zama na kizazi kilichopo ni cha utandawazi, ikifahamika vyema hasara za kutomchanja mtoto.

Cha muhimu katika yote, ni kufuata kanuni za afya zinazomuepusha mtoto na kizazi chake chote, dhidi ya maradhi hayo.

Wataalam wa afya, nao wana wajibu wa kuwaeleza wazazi wa watoto wanaopatiwa chanjo, namna ya kujikinga, faida na hasara zilizopo kwa kwa watoto wao.

Itapendeza kwa mzazi anayeenda kwenye kituo cha afya kuchanjwa, anarudi nyumbani wakiwa na ufahamu wa sababu zake, hali inayowapa moyo waliochanjwa waendelee kufuatiia huduma hiyo kwa hamasa ya juu.

## HABARI KITAIFA

# Ahukumiwa kunyongwa mpaka kufa kwa kumuua mama mkwe

**Na Joctan Ngelly, Geita**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza, imemhukumu Magina Ruhanga (51) kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia mama mkwe wake, Holo Budeba.

Ruhanga ametiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu hiyo baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi uliotolewa kwamba alimcharanga mama mkwe wake huyo na mapanga kisha kuchukua sehemu zake za siri na titi la kulia na kutokomea navyo kusikojulikana.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Jaji Agnes Mgeyekwa katika kikao cha Mahakam kilichoketi mjini hapa baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Mgeyekwa alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia ya kuua watu kwa kukusudia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani hapa mashahidi watano na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimuua mama mkwe wake kwa kumcharanga na mapanga.

Katika kesi hiyo upande wa mashtaka uliongozwa na Wakili wa Serikali Erasto Anosisye na upande wa utetezi wa mshtakiwa ulikuwa ukiongozwa na wakili wa kujitegemea Liberatus Rwabuanga.

Jaji alisema mshtakiwa aliamuua kumuua mama mkwe wake kwa madai kuwa alimzuia mtoto wake kurudi kwa mshtakiwa huyo, ndipo akafanya mchakato wa kuwatafuta watu wawili ambao walisaidiana naye kwa makubaliano ya malipo ya Sh. 400,000 na kabla ya tukio hilo aliwapatia Sh. 50,000 kwa ajili ya kununua mapanga na tochi eneo la Katoro.

Pia Jaji Mgeyekwa alisema ilipofika usiku, walikwenda katika kijiji cha Kanegere kisha kuvunja mlango na kuingia ndani ya chumba cha mama mkwe na kuanza kumcharanga mapango sehemu za kichwani kisha kukata sehemu za siri pamoja na titi la kulia na kuondoka navyo.

"Nimeangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa kitendo alichokifanya mshtakiwa huyu ni cha kikatili sana. Upande wa mashtaka umethibitisha kosa hili pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama hii inamhukumu mshtakiwa kunyongwa hadi kufa," alisema.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Msaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Renatus Kerenge, alidai kuwa Novemba, 2014 majira ya saa 5:00 usiku katika Kijiji cha Kanegere mkoani Geita, mshtakiwa alimuua Holo Budeba, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.




Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali watu cha Benki ya KCB, Fauqiya Shareef (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa benki hiyo, Christina Manyenye wakifurahi baada ya kushinda tuzo za wanawake viongozi (WIMA), zilizofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usajili VICOBA, SACCOS wapamba moto

**Na Salome Kitomari**

VICOBA 2,000 vimesajiliwa kwenye mfumo rasmi wa kidigitali ikiwa ni utekelezaji wa sheria ya huduma ndogo za fedha ambayo mwisho ni Ijumaa.

Aidha, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) 552 vimesajiliwa chini ya Mrajis wa vyama vya ushirika Tanzania.

Pia, kampuni na watu binafsi 807 wameomba kupewa leseni ya kuendesha shughuli hiyo, na kwa mujibu wa sheria ndani ya siku 60 watapewa ikiwa hakuna marekebisho.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilishia Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Victor Tarimu, alisema usajili utaendelea kwa watakaokidhi matakwa ya kisheria watapewa leseni.

Kuhusu malalamiko ya kushindwa kutumia mfumo, alisema kwa ujumla mfumo ni mgeni na kumekuwa na chagamoto ambazo zimetatuliwa na maofisa wa TEHAMA waliopewa mafunzo.

**MATAKWA YA KANUNI**

Kwa mujibu wa kanuni ya 4 hadi 7 ya mwaka 2019, watoa huduma ndogo za fedha, VICOBA vinatakiwa kufanya mkutano wa awali, kuwa na kamati ya mpito na majukumu yake na kikao cha uanzishaji na majukumu yake.

Kanuni ya 8 hadi 17 ni maombi ya usajili yakiambatana na nakala ya katiba yenye sahihi za wanachama, nakala za mihtasari ya mkutano wa uanzishaji, maazimio ya wanachama kuanzisha kikundi.

Vinatakiwa kuwa na mapendekezo ya muundo wa kikundi, uthibitisho wa malipo ya michango ya awali, barua ya mamlaka ya kata au kijiji, na jina la kikundi lijumuishe maneno 'kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii' na baada ya kukamilisha wanakikundi watatakiwa kufanya kikao cha kwanza ndani ya mwezi mmoja.

Kwa mujibu wa sheria hiyo kuna makundi manne ya usajili ambayo ni VICOBA vinavyosajiliwa chini ya usimamizi wa halmashauri, SACCOS chini ya Mrajis, Kampuni na watu binafsi pamoja na benki za huduma ndogo za fedha chini ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

# RC atoa agizo kuhusu vipimo

**Na Jumbe Ismaiily,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, ameipongeza Wakala wa Vipimo (WMA) kwa kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji kwa mkoa huo, na kuwaagiza viongozi wa mkoa kuhakikisha unafanyika utaratibu ili wataalam na watendaji wote wanaohusika na wazalishaji wapate mafunzo yanayohusiana na vipimo.

Dk. Nchimbi alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua mafunzo na elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji ambayo yaliwashirikisha wafanyabiashara wanaosindika mafuta na kufungasha bidhaa mbalimbali.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na WMA. "Ninawapongeza WMA kwa kutoa mafunzo haya hapa kwetu na ninamuagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida na wakuu wa wilaya zote kuhakikisha unafanyika utaratibu wa wataalamu wote wanaohusika na wazalishaji kupata mafunzo haya," alisema na kuongeza;

"Nataka kuona darasa la namna hii juu ya vipimo kwa watendaji wote, wakiwemo maofisa ugani, lazima wawe na majibu kuhusu vipimo."

Aliagiza sekretarieti ya mkoa huo na za wilaya kuhakikisha mafunzo hayo yanatolewa na katika maeneo yao na kwamba katika hilo, hakuna bosi.

"Bosi ni mzalishaji na yule anayetaka vifungashio vilio sahihi na tunaowatumikia ni wale wanaozalisha, wanaotafuta vipimo sahihi, wanaotafuta kuwa na vifungashio vilivyo sahihi, wazalishaji mkizalisha vizuri mkatumia vipimo sahihi na kuweka katika vifungashio vilivyo na ubora ndipo kutasaidia kuwepo uchumi uchumi imara."

Alisema muda sio mrefu anataka kuona mafunzo hayo kwa watendaji wote na yeye akiwamo, na kwamba katika hilo hakutakuwa na visingizio.

"Haiwezekani wawepo watendaji, watumishi na watalaam ndani ya mkoa na wilaya zetu halafu, tumsubiri mtu wa WMA kutoka Dar es Salaam au Dodoma kutupa mafunzo," alionya.

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.LAND APPLICATION NO 167 & 168 of 2019**
**MICHAEL M. NYAMIKA……...........…APPLICATION**
**VERSUS**
**TATU S. TULIENI & OTHERS………RESPONDENTS**
**TO: ERICK AUCTION MART & COURT BROKER………5TH RESPONDENT**
**NOEL ESTATE COMPANY LIMITED…………6TH RESPONDENT**
**P.O. Box……………**
**DAR ES SALAAM**

WHEREAS: The above named APPLICANT has institute the APPLICATION against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 24TH day of JUNE, 2021 at 9:00 AM Before Hon. DR. Z.D. MANGO, JUDGE, in the morning to answer the said SUIT, and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely in support of your REPLAY.

TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day the APPLICATION will be heard and determined in your absence.
Given under my hand the seal of this court, this 28th day of APRIL, 2021.

DEPUTY REGISTRAR

# Mabadiliko sheria ya uwekezaji yaja

Na Beatrice Moses

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Wiliam Ole Nasha, amewahakikishia wafanyabiashara na wawekezaji kuwa sheria mpya ya uwekezaji itakuwa tayari kutumika kabla ya mwisho wa mwaka huu, hivyo kuondoa kilio cha muda mrefu kwa wafanyabiashara nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao kazi cha pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kilioandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) wa kujadili rasimu ya mkakati wa maendeleo ya uwekezaji na mapendekezo ya sheria mpya uliofanyika jijini Dar es Salaam, Nasha alisema kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara na sasa suluhu ya kudumu imepatikana.

"Kwa muda sasa wafanyabiashara wamekuwa wakieleza changamoto zao za ufanyaji biashara nchini ikiwamo ucheleweshwaji wa vibali, urasimu, mazingira ya biashara yasiyotabirika pamoja na rushwa. Kama serikali tumekusudia kuja na sera na sheria mpya ili kuweka mazingira rafiki kwa wao kufanya biashara," alisema.

Alisema milango ipo wazi kwa wafanyabiashara kutoa mapendekezo yao ili kuleta sheria ambazo zitakuwa rafiki na kuchochea ukuaji wa soko la ajira kwa vijana na pato la taifa.

"Tuendelee kutumia majadiliano kama haya ambayo huandaliwa na TNBC kama njia sahihi za kufikisha changamoto zenu katika sehemu husika kwa kuwa chombo hiki kinaripoti moja kwa moja kwa Rais ambaye pia ni mwenyekiti wa TNBC," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema Baraza limejipanga vyema kwenda na kasi ya mabadiliko ya sera na sheria za ufanyaji biashara nchini.

"Jukumu la Baraza ni kuzileta pamoja sekta binafsi na umma ili kujadili changamoto za ufanyaji biashara na kuzifikisha kwa Rais ili zipatiwe ufumbuzi kwa haraka, tutaendelea kufanya majadiliano kuanzia kwenye mabaraza ya wilaya, mikoa na taifa kwa lengo la kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara," alisema Dk. Wanga.

Wilbard Chambulo, mfanyabiashara, mbali ya kuyapokea mabadiliko ya sera kwa mikono miwili, ameitaka serikali kuendelea kujenga imani na kuweka mazingira yanayotabirika ya ufanyaji biashara nchini.




Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi (kushoto), akizungumza na wafanyakazi wa kampuni ya sukari Kilombero, alipotembelea banda la kampuni hiyo, katika maonyesho ya wiki ya afya na usalama mahala pa kazi yaliyoandaliwa na OSHA, jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkenda awaonya polisi

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, amepiga marufuku Jeshi la Polisi kukamata wafanyabiashara ya mahindi wakati wanapeleka bidhaa hiyo sokoni, akisisitiza kuwa tabia hiyo inawavunja moyo wakulima.

Amesema anatarajia kuzungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) kuhakikisha jeshi hilo linaachana na tabia ya kukimbizana na wafanyabiashara hao wakati wakipeleka biashara zao sokoni.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea mashamba ya kilimo cha mkataba wa zao la mtama wilayani Kongwa juzi, waziri huyo alisema kumekuwa na tabia ya askari polisi wanapoona gari limebeba mahindi, wanaanza kukimbizana kuyakamata na kuyazuia kuendelea safari kana kwamba gari hilo limebeba bangi.

"Kuna changamoto kubwa ya masoko inayowakabili wafanyabiashara wa mahindi nchini, wafanyabiashara hao wana uhuru wa kufanya biashara eneo lolote nchini kwa kuwa wanakuwa wakitafuta masoko, hivyo kuwazuia na kuwanyang'anya mazao yao wakati wakipeleka sokoni ni kuwavunja moyo na kuwakatisha tamaa," alionya.

Prof. Mkenda aliwataka askari wa Jeshi la Polisi kuacha tabia hiyo ya kuwasumbua wakulima na wafanyabiashara wa zao hilo ambao wanakuwa wakipambana kujikwamua na umaskini na kuchangia pato la taifa.

"Hiki kitu kwa kweli siyo kizuri, hawa ni Watanzania ambao wanatafuta masoko ya zao hilo, ni vyema wakaachwa ili kuendelea na biashara hiyo," alisema.

Katika hatua nyingine Prof. Mkenda aliwataka maofisa ugani kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wa mazao mbalimbali wilayani humo ili wafanye kilimo chenye tija ambacho kitaleta matokeo chanya kwao na taifa kwa ujumla.

Waziri huyo alisema kilimo ni sekta muhimu ambayo ikifanywa kwa kuzingatia kanuni kuanzia kupanda, hususani mtama, mkulima atapata mavuno mengi ambayo yatachangia kupata fedha nyingi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sagara B wilayani Kongwa mkoani Dodoma, Gilbert Mlwande, alimshukuru waziri huyo huku akisema amewasaidia wakulima na wafanyabiashara kutatua kero ya kukimbizana na askari polisi barabarani.

Alisema hivi sasa wanakwenda kufanya biashara hiyo bila kuwa na bugudha yoyote kutoka kwa vyombo vya usalama barabarani.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Seleman Serera, alisema wakulima wa Kongwa wana shauku kubwa ya kuendesha kilimo cha mkataba cha zao la mtama pamoja na kilimo cha mazao mengine kitaalamu ili kusonga mbele katika kilimo.

Dk. Serera alisema ujio wa wawekezaji hao wa ndani utawafanya wakulima wa Kongwa kufanya kilimo cha kisasa ambacho kitaleta manufaa makubwa kwa wakazi wa eneo hilo na taifa.

# Zaidi ya mawakili 200 hawajulikani

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Tanzania imetoa majina ya mawakili 298 ambao hawajahuisha taarifa zao binafsi na kuweka maelezo muhimu katika akaunti zao kwenye mfumo wa mawakili Tanzania.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa katika moja ya magazeti na Mahakama Kuu, likiwa na orodha ya majina ya mawakili hao, ambao wanatakiwa kujiandikisha kwenye mfumo wa Tanzania Advocate Management System (TAMS), ambao wameainishwa kama mawakili wasiojulikana.

Tangazo hilo lilibainisha kuwa mawakili hao wameendelea kuwapo kwenye orodha ya wanachama wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), bila kuhuisha taarifa zao kama sheria inavyotaka.

"Kukosekana kwa taarifa hizo muhimu pamoja na kufahamika wako wapi, kumepelekea kutokuwapo kwa taarifa zao binafsi kwenye mfumo wa mawakili Tanzania pamoja na kanzi data ya mawakili," lilibainisha tangazo hilo.

Aidha, tangazo hilo lilisema uwapo wa taarifa sahihi za wakili anayehusika katika TLS na Ofisi ya Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania kunawapa fursa wadau wote na wananchi kwa ujumla kuwafahamu mawakili walioruhusiwa kufanya kazi za uwakili.

"Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia Ofisi ya Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania inautangazia umma kwamba mtu yeyote ambaye taarifa za wakili au anafahamu chochote kuhusu wakili yeyote aliyeorodheshwa atoe taarifa," ilisema taarifa hiyo.

# Wadau wakubaliana na Samia Benki ya Kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi wamepongeza hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan iliyoelezea mpango wa serikali ya kuiongezea fedha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili iweze kutoa mikopo mingi zaidi kwa riba nafuu, sambamba na kuchangia ukuaji na maendeleo ya sekta hizo pamoja na viwanda.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau wameelezea matumaini yao makubwa kuwa TADB ikiwezeshwa zaidi, mchango wake katika maendeleo na ukuaji kwa sekta husika utaongezeka maradufu ikiwemo kuimarisha ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini.

Christian Ngatunga, mkulima wa soya na mahindi katika Wilaya ya Songea Vijijini, alisema mpango wa kuongezea nguvu TADB ufanyike mapema ili msimu ujao wa kilimo uweze kuwanufaisha wakulima wengi.

"Hatua hii inaonyesha dhamira ya kweli ya serikali ya kuendeleza na kuinua sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ambapo TADB imekuwa ikitoa mikopo kwa zaidi ya miaka mitano sasa, hivyo ikiongezewa fedha itaweza kuchochea ukuaji wa kilimo na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao," alisema Ngatunga.

Alisema tija ya kuongeza uzalishaji wa mazao unategemea na uwekezaji mkubwa kwenye maandalizi ya shamba na matumizi ya zana bora za kilimo, hivyo wakulima wakiwezeshwa mikopo kupitia TADB, kutakuwa na mapinduzi ya kilimo nchini na kuchangia sehemu kubwa katika pato la taifa.

Akihutubia Bunge kwa mara ya kwanza Alhamisi, Rais Samia aliwaeleza Watanzania kuwa serikali ya awamu ya sita imekusudia kuongeza fedha katika TADB ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Alieleza kuwa kilimo kinachangia asilimia 100 ya chakula nchini, asilimia 60 ya malighafi za viwandani, asilimia 27.7 ya pato la Taifa, na asilimia 25 ya fedha za kigeni, huku changamoto kubwa ikiwa katika upatikanaji wa mitaji, mbegu bora, hivyo nguvu kubwa itaelekezwa kwenye tafiti za mbegu bora, na kuwekeza zaidi TADB ili iweze kutoa mikopo yenye riba nafuu zaidi kwa wakulima, wavuvi na wafugaji..

Joel Elinasha, mkulima wa shayiri kutoka Kiteto mkoani Manyara, alieleza kufarijika na hotuba ya Rais Samia kwani imejaa maono makubwa hususani katika swala la utafiti wa mbegu bora ambao utawezesha kuongezeka uzalishaji wa mazao.

Naye Benson Shija, mfugaji kutoka Bariadi, mkoani Simiyu, alisema yupo tayari kujifunza njia bora ya ufugaji wa kisasa na kuachana na ufugaji wa kuhamahama kama alivyoeleza Rais Samia katika hotuba yake, lengo ni kuifanya sekta ya ufugaji kukua na kuchangia sehemu kubwa katika pato la taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alimshukuru Rais Samia kwa kutambua mchango wa TADB katika ukuaji wa sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, huku akisisitiza kwamba benki hiyo itaendelea kutoa mchango mkubwa katika sekta hizo ili kuweza kuwanufaisha wakulima wengi zaidi.

"Mpaka Desemba 2020, TADB imeshanufaisha wakulima 1,788,202 na kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 300 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mikopo hii imewezesha kukua kwa minyororo ya thamani kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi," alisema Justine.

"Hivyo, hotuba ya Rais imetuongezea nguvu zaidi, na sisi kama benki tunaahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa bidii ili kufikia dira ya Rais katika eneo la kilimo, ufugaji na uvuvi kama aliyoelezea kupitia hotuba yake," alisema Justine.




Ofisa Mauzo wa kampuni ya bidhaa za Solar ya D.light Mkoa wa Mwanza, Seif Mweta, akitoa maelezo ya bidhaa zao kwa wakazi wa Jiji la Mwanza, wakati wa uzinduzi wa ofisi ya Kanda ya Ziwa, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali, w'biashara sekta ya mafuta ya kula wanolewa TBS

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limeendelea kutoa mafunzo maalum kwa wajasiriamali 282 na wafanyabiashara kwa ujumla wanaojishughulisha na sekta ya mafuta ya kula.

Wafanyabiashara hao wanatoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na Halmashauri ya Mji ya Gairo za mkoani Morogoro.

Mafunzo haya maalum yamewalenga wajasiriamali na wafanyabiashara wanaojishughulisha na uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa mafuta ya kula katika masoko ya ndani na ya nje katika Mkoa wa Morogoro.

Akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, Meneja wa Utafiti na Mafunzo wa TBS, Hamisi Mwanasala alisema mafunzo haya ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika sambamba na agizo la Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kulitaka Shirika kuendesha mafunzo haya maaalum mikoa yote.

Sudi alisema Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wajasiriamali ikiwa ni pamoja na wanaojishughulisha na sekta ya mafuta ya kula katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema mafunzo haya ni mahsusi kuwajengea uwezo wadau wa mafuta ya kula nchini ili waweze kuzalisha mafuta kwa wingi na yenye ubora unaokidhi matakwa ya viwango vya mafuta ya kula.

"Mafunzo haya yataenda sambamba na utoaji wa elimu kwenye masoko na vituo vya pembezoni mwa barabara ambapo wauzaji wengi wanauza mafuta ya kula," alisisitiza," alisema Sudi.

Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Gudila Boniface, alisema ili mafuta ya kula yakidhi viwango ni lazima kufuata kanuni za kilimo bora, usindikaji na usafi.

Gudila alisema kanuni za kilimo bora zinahusisha matumizi ya mbegu bora, kuvuna kwa wakati mazao yalikomaa.

Kwa upande wa kanuni bora za usindikaji kwa mujibu wa Gudila ni pamoja na kutumia malighafi bora, vifaa vya kusindikia ambavyo havishiki kutu na vilivyoshauriwa na wataalamu.

Akizungumzia kanuni bora za usafi, Gudila alisema wazalishaji wanatakiwa kuhakikisha vifaa vya kuhifadhi mafuta ni safi ikiwa ni pamoja na madumu yanayotumika kuhifadhi mafuta hayo yawe yamesafishwa vizuri pamoja na usafi wa mazingira.

Aidha, alisema mafuta ya kula hayatakiwi kuwekwa juani, kwani yanapokuwa juani kuna kemikali zinazozalishwa na zinaweza kusababisha mafuta kuharibika ambayo yakitumiwa na walaji yanaleta athari za kiafya.

# W/biashara kutoka nje waonywa udanganyifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amewaonya wafanyabiashara kutoka nchi za jirani wanaonunua bidhaa za Tanzania na kisha kuweka nembo za nchi zao ili kuonekana zimetoka kwao na kuzisafirisha nje.

Macha aliyabainisha hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa wajasiriamali 100 wa bidhaa ya mchele Kanda ya Ziwa yanayoendeshwa na Shirika la Viwango Nchini (TBS).

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa na wachakataji wa ndani kwa kushirikiana na wafanyabiashara kutoka nje.

Alisema kuwa kitendo cha baadhi ya wafanyabiashara kutoka nchi za jirani kuja kununua mchele kwa kutumia vifungashio vyao kutoka nchi wanazotoka vinashusha soko la ndani na nje na kuonesha nchi hizo zinazalisha mchele kwa wingi jambo ambalo sio la kweli.

"Tusiruhusu wafanyabiashara kuja na kutumia vifungashio vyao kwenye bidhaa tunazozichakata viwandani kwetu, tuwauzie mchele tulioufunga kwenye vifungashio vyetu tulivyotengeneza wenyewe ili kukuza biashara zetu na watakapokwenda kubadilisha dhambi iwe juu yao," alisema Macha.

Alisema wengine wamekuwa wakinunua mchele moja kwa moja shambani kwa mkulima kwa bei ndogo ikilinganishwa na bei ya soko na kuhifadhi kwenye maghala ya wafanyabiashara ili kuuza baadaye kwa bei ya juu.

Kwa upande wake, Meneja Mafunzo na Utafiti kutoka TBS, Hamisi Mwanasala, alimpongeza mkuu wa wilaya kwa kuendelea kupambana na wafanyabiashara wanaokuja nchini na vifungashio vyao.

Aliwataka wasindikaji kuzalisha bidhaa hizo kwa ubora unaohitaji na kufunga kwenye vifungashio vinavyohitaji na vyenye nembo ya TBS ili kukuza masoko.

# Sheria upandikizaji viungo yaja

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa katika mkutano wa Septemba mwaka huu, serikali itawasilisha muswada wa kutunga sheria itakayoongoza taratibu za uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa viungo kwa wenye uhitaji.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Rose Tweve (CCM).

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itapeleka bungeni muswada huo ili kuharakisha upatikanaji wa viungo hivyo.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema kwa sasa mchakato huo uko katika hatua ya ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau na katika mkutano ujao muswada huo utawasilishwa bungeni.

Katika swali la msingi, Tweve alihoji serikali ina mkakati gani wa kuanzisha utaratibu maalum wa kuvuna viungo kama vile figo na moyo kwa ajili ya Watanzania wenye uhitaji wa viungo hivyo.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema kwa sasa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa zinatoa huduma za uvunaji na upandikizwaji wa figo nchini tangu Novemba 2017 kutoka kwa wachangiaji walioridhia.

"Hadi sasa, Hospitali ya Taifa Muhimbili imepandikiza figo 62 na Hospitali ya Benjamin Mkapa imepandikiza figo 18 na kwa upande wa upandikizaji wa moyo, serikali inaendelea kujenga uwezo wa ndani wa kutoa huduma hii," alisema

Alisema kwa kuwa huduma zimeshaanza kutolewa, kwa sasa nchi inatumia miongozo ya kimataifa inayosimamia uvunaji na upandikizaji wa viungo.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akiteta jambo na Naibu wake, Khamisi Hamza Chilo, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mfumo utambulisho mazao waandaliwa

SERIKALI kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha biashara imeandaa mfumo maalum wa kutambulisha mazao ya viungo yanayozalishwa Tanzania katika masoko ya ndani na nje.

Vilevile, serikali itaendelea kusimamia mikakati yote inayolenga kuongeza uzalishaji, tija na kuboresha mazingira ya biashara ya zao la vanilla na mazao ya viungo ili kuongeza hamasa kwa wakulima kuzalisha mazao hayo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Maryam Azan Mwinyi (CCM).

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali katika kuhamasisha uzalishaji wa zao la vanila nchini.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema zao la vanila hulimwa kwa wingi katika mikoa ya Kagera, Morogoro, Tanga, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro ambapo uzalishaji umekuwa ukiongezeka kutoka tani 229.8 mwaka 2015/16 hadi kufikia tani 1,949.80 mwaka 2019/20.

"Katika kuhamasisha uzalishaji wa zao la hilo, Wizara ya Kilimo imefanya tathmini ya kutambua wadau na masoko ya vanila ndani na nje ya nchi na kuzifahamu changamoto zinazokabili zao hilo ikiwamo upatikanaji wa mbegu bora," alisema.

Bashe alisema wadau wakubwa wa vanila ni pamoja na Shirika la Msalaba Mwekundu, Umoja wa Wazalishaji wa Viungo (TASPA), Chama cha Wakulima wa Viungo Amani Tanga (CHAVIA), Chama cha Maendeleo ya Wakulima (MAYAWA), Taasisi ya Kilimo Endelevu (SAT), Ushirika wa Wazalishaji Viungo wa Mtamba Morogoro, Kiwanda cha Natural Extract Limited kilichoko Kilimanjaro na Chama cha Wazalishaji Vanila mkoani Kilimanjaro.

Alisema serikali itaongeza upatikanaji wa miche bora ya vanila nchini kwa kuhamasisha wazalishaji wa ndani na kuandaa utaratibu wa kuingiza miche bora kutoka Uganda.




"Pia, serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuhamasisha uendelezaji wa zao la vanilla na mazao mengine ya viungo kwa kutoa mbinu bora za kilimo cha vanila, kuanzisha vyama vya wakulima na majukwaa ya wadau ili kujadili maendeleo ya tasnia ya viungo," alisema.

Alisema kuwa hadi kufikia Machi 2021, jumla ya wakulima 1,387 wa wanila walikuwa wamepatiwa mafunzo ya kanuni na mbinu bora za uzalishaji.

"Katika kuimarisha huduma za ugani kwa zao hilo, maofisa ugani 20 wamepatiwa mafunzo, Kituo cha Utafiti TARI - Tengeru kinafanya utafiti wa mazao ya bustani likiwamo zao la vanila na viungo.

"Kituo hicho kimeanza ukusanyaji wa vinasaba vya mazao likiwamo zao la vanilla kwa ajili ya kufanya utafiti wa aina bora za vanila ili kuboresha uzalishaji," alisema.

# Sababu wanyamapori kuvamia mashamba

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema shughuli za kibinadamu kwenye shoroba, maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori na maeneo ya kinga ya Hifadhi ya Ngorongoro, zinachangia kuwapo kero ya wanyamapori kuingia kwenye mashamba yaliyoko pembezoni mwa hifadhi.

Naibu Waziri, Mary Masanja, alibainisha hayo bungeni jijini Dodoma jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso) CHADEMA).

Mbunge huyo alisema wananchi wanaoishi jirani na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wilayani Karatu, kwa muda mrefu wamekuwa wakipata adha kubwa ya wanyama kuingia na kuvamia mashamba yao na wakati mwingine kujeruhi wananchi.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo hilo?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masanja alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, wizara inatoa rai kwa wananchi kutumia mbinu mbadala za kuepuka wanyamapori wakali na waharibifu kuingia kwenye maeneo yao.

Alitaja mbinu hizo kuwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki kwenye mipaka ya hifadhi zilizokaribu na maeneo ya vijiji ili kuhakikisha wanyamapori hawavuki kwenda kwenye mashamba.

"Wananchi wanahamasishwa kulima zao la pilipili kandokando ya mashamba yao kwani zao hili limeonekana kuwa ni tishio kwa wanyama wakali na waharibifu kama tembo," alisema.

Pia, alishauri wananchi kutopanda mazao yanayovutia tembo kusogea katika mashamba yao kama vile katani, miwa, ndizi na matikiti na kuendelea kutumia oil chafu iliyochanganywa na pilipili na majivu ili kuzuia wanyama kama tembo kusogea kwenye maeneo ya mashamba.

"Mbinu nyingine ni wananchi wanashauriwa kutoa taarifa haraka pindi wanyama hao wanapoonekana kukaribia kwenye mashamba yao,"alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na kero za kuongezeka kwa matukio mbalimbali ya wanyama wakali na waharibifu wakiwamo tembo, wizara imeongeza idadi ya vituo vya muda na vya kudumu vya askari katika maeneo yaliyohifadhiwa likiwamo eneo la Ngorongoro na kuendelea na doria za usiku kuhakikisha wanyamapori waharibifu wanarudishwa hifadhini.

ama
ALHAMISI APRILI 29, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**UGONJWA UBONGO KWA WATOTO WENYE MADHILA HAYA, WAKINYIMWA FURSA SHULE**



**Ulivyo mlipuko wa corona India na magumu ya ‘ndugu zetu’ walionasa**

Ukurasa 13

# Wadau tiba waja na njia mbadala ya kumpata daktari bingwa ‘kimtandao’

**Na Yasmine Protace**

KATIKA mustakabali wa kawaida, asilimia kubwa ya wafikao hospitali, zahanati au kwenye kituo cha afya, lengo lao kuu ni kupata matibabu.

Hapo nako huwa kuna azma zinatofautiana. Wako wanaofuata tiba za kawaida, wengine haja ya huduma za kibingwa, hususan madaktari.

Ni kupitia dhana hiyo ya mwisho, kunapatikana ugumu wa pili, mtu anakutana na foleni ndefu kumuona mtaalamu huyo, bado anaweza asifanikiwe.

**NAMNA WANAVYOTATUA**

Nini kinafanyika? Hapo ndiko kuna njia ya kumwepusha foleni hasa anayetaka kumuona tabibu bingwa. Kumebuniwa njia rahisi ya mtandao kutoa

kisima cha majibu kwa magumu kutoka tasnia ya afya, kwa wenye uhitaji.

Mkurugenzi wa asasi mpya ya Afyayangu, Dk. Cyprian Ntomoko, anasema katika uzinduzi wa njia hiyo ya mawasiliano, iitwayo PASEDO, kwamba lengo kuu ni kukabili magumu yaliyoko ndani ya tasnia ya afya.

Hapo anajigamba atawagusa wenye uhitaji kwa namna bora, nafuu na inayojali muda, kukipatikana majibu yenye suluhu kwa matatizo mbalimbali ya kiafya na



Mkurugenzi Mtendaji wa Afyayangu, Dk. Cyprian Ntomoko, alipozungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuzindua asasi ya Afyayangu. **PICHA: YASMINE PROTACE**

mengineyo wanayohusiana nayo.

“Moja ya sababu ya watu wengi kuteseka na aina fulani ya ugonjwa ni kuchelewa kutafuta au kupata huduma sahihi ya matibabu. Hiyo inachangiwa na kutokujua wapi mahali sahihi ya kupata huduma au namna ya kufika kwenye kituo husika,” anafafanua.

Dk. Ntomoko anaeleza namna wagonjwa wengi wanavyoogopa foleni na usumbufu wa hospitalini, pindi wanapohitaji huduma au wanapopenda kutibiwa katika hospitali waitakayo na daktari wanayemlenga, huwa wanakwama.

Anasema majibu ya madhila ya aina hiyo kiafya ni katika miradi ya asasi Afyayangu iliyobuni mbinu ya kumkutanisha tabibu na mgonjwa. kupitia kituo cha kutoa huduma na watoa huduma (madaktari) kwa njia rahisi inayotumia teknolojia iitwayo PASEDO.

Kwa mujibu wa Dk. Ntomoko, unatarajiwa kuwa mwarobaini wa upatikanaji huduma za afya katika maeneo tofauti nchini na kwa wakati mwafaka

Anaahidi teknolojia ya PASEDO, itamuwezesha daktari au mtoa huduma, kutumia kipawa na ujuzi alionao kuwahudumia wahitaji kwa sababu PASEDO itamsaidia.

Anafafanua kwamba, ni aina inayowapata wagonjwa wa kutosha na wanaohudumiwa kwa wakati, kuepusha upotezaji muda wa daktari kuwasubiri wagonjwa.

Pia, anasema PASEDO inarahisisha kujenga tafsiri ya namna wateja wanaomwamini wanakusanyika na kufikika wakiwa wenye furaha na huduma waipatayo.

Ahadi yake kimuundo, anasema ni kuipangilia kliniki vizuri na katika uendeshaji wake, kunatarajiwa kuweka utaratibu rafiki wa miadi ya wagonjwa, ili kutowapotezea muda na kupata fursa ya kuboresha huduma za afya, kwa mujibu wa walichokipanga.

Hadi sasa ‘Afya Yangu’ imedhamiria kutumia teknolojia hiyo, iguse kila eneo linalohusu afya katika maeneo kama vile; dawa, vifaa tiba na mazoezi tiba.

“Hivyo basi, ninawaomba Watanzania na wananchi kwa ujumla hasa wanaoishi mkoa wa Dar es Salaam, ambako ‘PASEDO App’ inaanzisha mtandao wake,” anasimulia Dk. Ntomoko

Lingine, anawahimiza madaktari na watoa huduma wote, wajisajili na mtandao huo, pamoja na vituo vya kutoa huduma za afya.

Mshiriki wa tukio la uzinduzi, Mwajuma Ally, anasema utawasaidia watu waliokwishazoea kwenda hospitali kupata matibabu na wakati huohuo, upatikanaji wa daktari bingwa umekuwa kitendawili kupatikana kirahisi.

Anasema mfumo huo utawasaidia watu wengi kabla ya kwenda hospitali kuanza kumtafuta huyo unayetaka kumuona na utafanikiwa kumuona.

Mwajuma anaeleza maoni yake, akitamka:”Mfumo huo utakuwa mkombozi, kwani mtu atatoka nyumbani na atakuwa anajua unaenda kumuona ambaye anamtaka kumuona.”

Sadiki Jamal, mkazi wa Dar es Salaam, akiwa mdau wa uzinduzi wa mpango huo, anakiri tamko la mwenzake, Mwajuma, kwamba mfumo utasaidia kuwapunguzia watu kukaa foleni ya muda mrefu, wakijipanga kwa utaratibu wa kumwona daktari.

AFYA

UNAUJUA USONJI?

# Ugonjwa wa ubongo kwa watoto wenye madhila haya, wakinyimwa fursa shule

## •Daktari: Nawapigania nje, kwangu 'nimechemka'

**Na Romana Mallya**

UNAPOTAJA Usonji una maana gani? Ni tatizo linalowapata watoto katika mfumo wa fahamu na kuwasababishia matatizo ya kutengeneza uhusiano na jamii.

Huwa wanategeneza mawasiliano kwa maneno, ishara au vitendo na tabia ya kujirudia. Mpaka sasa haina tiba na dalili zake zinaonekana kuanzia umri chini ya miaka mitano.

**INAUGUSAJE UMMA?**

Hapo kuna, simulizi zinazobeba huzuni, ndani yake ikisheheni ujumbe mzito kwa jamii, serikali na wadau wengine, zikilenga kuwezesha watoto walio na usonji, wapate haki ya elimu kuanzia chini hadi ngazi za juu.

Ilikuwa tarehe 10, mwezi huu, wastani wa wiki mbili na nusu sasa, wazazi wa watoto wenye usonji walikutana jijini Dar es Salaam kupaza sauti za kutaka mtoto wenye tatizo hilo wapatiwe fursa ya elimu, kwani hadi sasa wanadai ni sintofahamu, wakipitia kaulimbiu ya mwaka huu "Elimu Jumuishi, Jamii Jumuishi, Kazi Jumuishi."

Mkurugenzi wa Kituo cha Afya cha THT, Dk. Isaac Maro, ni miongoni mwa wazazi walioanika magumu ya watoto wao, akisimulia anavyoshiriki kuwasaidia wengi katika jamii baada ya kazi, bila wengine kujua naye alikuwa na lake.

"Mwaka 2012 Mungu alinibariki nikapata mtoto wa pili. Mwenyewe daktari nikafurahia, nimekaa naye, lakini wenzake wakigombania kuangalia katuni, yeye yupo anafanya mambo yake. Mama yake anampenda kweli kwa sababu gani, alikuwa hasumbui!

"Yaani 'dogo' ukimuacha sehemu unamkuta hapo hapo. Akichukua 'katrei kake' wenzake wakimnyang'anya wala hajali. 'Kimoyo moyo' nikawa nasema hapa kuna kitu...." anasimulia.

Anasema kuna siku alikubaliana na mwandaaji kipindi cha televisheni anachoendesha kuzungumzia afya ya watoto na walikubaliana mada 'Afya ya Akili Kwa Watoto.'

Dk. Maro anaendelea kusimulia: "Kuna siku nyumbani kwangu nikaandaa mpira wa watoto uliojumuisha watoto wa mtaa. Watoto wote wakawa wanacheza, lakini wa kwangu amekaa chini.

"Wenzake wakicheza wakati mwingine anakwenda kukaa golini, nikabadili nikawaambia waje tupige picha, watoto wote waliangalia kamera, yeye wala!..."




Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Beatrice Fungamo (kushoto), alipozungumza kwenye matembezi ya hiari ya kuadhimisha Siku ya Watoto Wenye Usonji yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Anasema, baada ya majaribio kadhaa, ndipo akaona sasa anapozungumzia kitu kigeni kwa mtoto wake, ni ugonjwa usonji, hivyo alimpeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Daktari alipomwangalia, akasema tusubiri. Lakini nikamwambia, hapa suala hapa ni kuwahi. Ilinichukua miezi sita kukubali nina mtoto mwenye usonji.

"Haikuwa rahisi. Ninamshukuru Mungu kwa sababu alinifanya nikaujua zaidi usonji, nikausoma. Wakati fulani Mungu akabariki nikaenda shule nchini Japan, nikasema hapo ndiyo kwa kumponya mtoto, nikambeba nikaenda naye ili kutafuta namna ya kumuokoa," anasimulia mkasa.

Dk. Maro anasema, alipokuwa jijini Tokyo, Japan alifanya utafiti kwenye shule zenye watoto wenye usonji, akakuta wanachokifanya siyo kama kinachofanyika Marekani, wanaotoa dawa.

**NINI BAADAYA HAPO?**

Baada ya kubaini mtoto wake hawezi kupata dawa ya tatizo alilonalo, walirudi nchini na ndipo alipoingia kwenye mtihani wa pili.




Baadhi ya watoto wenye usonji. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Dk. Maro anasema akiwa nchini, walianza kutafuta shule mtoto wake apate haki hiyo kama wengine. Anaendeleza simulizi:

"Wazazi wote hapa wenye watoto wenye usonji wanajua elimu ya awali haina shida kwao kuipata. Watoto watapokewa kwenye shule za awali na watasoma, lakini watoto wetu wanakua.

"Binafsi nilimpeleka mtoto wangu katika shule ya dada (anamtaja), mpaka kiti hakimtoshi tena. Yaani peke yake ndiyo mkubwa darasani, sina pa kumpeleka tena, mwenye shule ananiambia mtoto hamtaki.

"Changamoto ikarudi tunakwenda wapi? "Mpaka sasa ninavyozungumza, ni hiyo hiyo na itaendelea kuwa hiyo hiyo na sasa ana umri wa miaka tisa, tunajiuliza watoto wetu wanakwenda wapi?" anahoji.

Swali la aina hilo liliulizwa pia na mzazi mwingine wa mtoto mwenye usonji, Mony Teri, anayeanika kiu yake kuona kundi hilo linapata fursa ya elimu hadi vyuo vikuu.

Mony ni Mwenyekiti na Mwanzilishi wa taasisi ya Pearl of People with Down Syndrome Tanzania, inayohusika na wenye mtindio wa ubongo, akiwataka wasiachwe kwenye vitengo pekee, bali wapatiwe fursa kujumuika na wenzao shuleni, kwa masharti yasiyojali mitihani.

"Mtaala umuwezeshe kujumika na wengine wa sekondari ili kuwe jumuishi. Wanaweza kufanya mambo mengine mengi, lakini siyo ya kimasomo, hawa wana ujuzi.

"Samwel Mwanyika ni kijana mwenye usonji, alipata Tuzo ya Kimataifa Mwaka 2017, baada ya kuonyesha ujuzi wake kupiga picha ya Zebra, katika Hifadhi ya Taifa Ngorongoro.

"Aliweza kumwona Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na tuzo yake. Mtoto wangu, Penny Pettit (26) anapenda kuogelea, kucheza, kuchora na kupiga ngoma. Wanapopewa fursa ya kukutana na vitu tofauti wanajifunza, wajumuishwe na washirikishwe," anasimulia.

Mony anaeleza hayo mbele ya Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo.

Mama huyo, pia anawavutia wazazi na walezi wenzake akiwatia moyo, baada ya kueleza namna binti yake alisoma hadi darasa la saba, na hadi sasa hajapata mwendelezo zaidi kielimu.

"Familia tulichukua hatua kumpeleka Uingereza kuendelea na masomo ya sekondari na chuo kinachofundisha namna ya kujikimu kimaisha," anasema.

Mzazi, Cecilia Meshy, mwanzilishi wa Mtandao wa Wazazi Wenye watoto Wanaoishi na Usonji, anazungumzia akiitacho 'Elimu, Jumuishi, Jamii Jumuishi na Kazi Jumuishi' kwamba wanahitaji walimu wanaoelewa suala hilo.

"Tunahitaji kuwa na jamii iliyopata elimu ya kutosha kuhusiana na usonji. Mzazi unaweza kuwa huru kutoka na mtoto wako," anafafanua mtazamo wa wazazi hao.

Anaendelea: "Lakini wazazi wanaowaficha watoto wao hawafanyi hivyo, kwa sababu wanajua wana mtu ambaye jamii haijamjua na hajamkubali,"

Cecilia anasimulia mkasa wake, kwamba alihangaika kuukubali ugonjwa na usonji kwa mtoto wake mwenye umri wa miaka miwili na miezi saba na akadokeza mageuzi yaliyombadilisha.

"Baada ya kuikubali hali hii, ilikuwa rahisi kwenda kokote na mtoto wangu, hata unapompeleka shule, unajaribu kumuelewesha mwalimu udhaifu wake na uwezo wake.

"Kwa upande wa elimu, changamoto tuliyo nayo usonji upo wa aina nyingi. Kama mzazi ukiweza kugundua mtoto wako ana usonji wa aina gani na kuubeba kwa sababu jamii haiwezi kukubali kitu ambacho wewe mzazi haujakikubali," anasema.

Mama huyo anasema nafasi yake ya mzazi anayempenda mwanawe, ndio njia ambayo jamii nayo inaweza kukubali na kuelewa kupitia kwao.

"Kanisani nilikuwa nakwenda misa ya wakubwa, lakini niliamua kwenda ya watoto, kwa sababu watoto wa usonji wanajifunza kwa

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Ulivyo mlipuko wa corona India na magumu ya Waafrika waliokwama



Dk. Edward Onantwa, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya, anayetibiwa nchini India. **PICHA: MTANDAO**.

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOFUATILIA kinachojiri katika kasi ya kusambaa maradhi ya corona duniani, nchini India, taifa lenye umma wa wakazi wengi, kasi yake ni kubwa kutisha.

Hadi juzi palishuhudiwa maambukizi ya wagonjwa 300,000 kwa siku, huku Jumapili pekee, palithibitishwa kufariki watu 2,767.

Ni jambo linalotokea, huku nchi hiyo ikiwa katika historia ya kupata ugeni mkubwa wa pande mbalimbali duniani; kitaaluma ikiwamo teknolojia ya mawasiliano ya habari, hali kadhalika wapo wanaofuata tiba mahsusi hospitalini.

Kwa janga corona, hadi sasa hospitali zimeelemewa na idadi ya wagonjwa Corona India na maambukizi ya virusi inatajwa kuvunja rekodi kimataifa.

Hospitali ya jijini New Delhi na nyingine nyingi, sasa zatajwa kuelemewa wagonjwa wahanga wa mlipuko wa corona, hali inayowalazimu watu kufanya mipango ya wagonjwa kutibiwa nyumbani.

Chanzo cha mlipuko ni nini? Joshua Boit, ni kiongozi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Kenya nchini India, anayesema kulikuwapo sherehe ya kidini nchini India iitwayo 'Kumbh Mela,'

Anasema, jumuiko lake iliwafanya watu wengi kukusanyika bila ya kufuata masharti ya mamlaka za afya, na ndio sasa inalaumiwa kuchangia kasi ya kusambaa virusi vya corona.

**WAAFRIKA WATAPATAPA**

Katika hizo safari za watoka Afrika Mashariki, wana simulizi za kilichowakuta huko, iwe matibabu au masomoni.

Akiwa katika mji wa Calcutta, Dk. Edward Onantwa, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kenyatta nchini Kenya, anasema madaktari wengi nchini India, wakiwamo waliofaa kumsaidia wamelazimika kutumikia kuwasaidia wagonjwa wa Corona

Dk. Onantwa, aliyedai kuwa India kwa miezi minne kutibiwa saratani, anasema amefaulu kupata matibabu, ingawa ana lake lakini janga la Corona na la sura ya pili, kuzuka corona kumeathiri ubora wa huduma alizopewa .

Anasema, akiwa mjini Culcuta, alishuhudia namna madaktari wengi wa India, kujumuisha anaowataja 'waliofaa kumpa matibabu' wamelazimika kutumiwa kuwasaidia wanaoumwa corona.

Ni katika hiloanasema, gharama ya matibabu imeongezeka na jinsi corona linavyoielemea India, amekutana na kikwazo kipya katika kupata tiketi ya ndege kurejea nyumbani Kenya.

Kwa mujibu wa mwanazuoni huyo wa Chuo Kikuu Kenyatta, hali iliyoko ni mbaya kuliko taarifa inayosambaa, hata wagonjwa wana hofu ya kuambukizwa corona, wakati wa kuonana na daktari, hisia ambazo pia zinamgusa tabibu.

Hilo kwake Dk. Onantwa analalamika, kwamba ni mtihani mwingine, ikizingatiwa inazuia kupumua vizuri, ilhali ana tatizo la kifua.

Pia, anasema mipuko wa corona umemdhibiti kitabibu, kwamba anapaswa kufanyishwa mazoezi ya kila mara, hali iliyoshindikana.

Malalamiko yake mengine, ni kwamba madaktari wengi walioukuwa wakimshughulikia, sasa wanatakiwa kutoa msaada kwa wagonjwa wa corona.

**WANAFUNZI WAAFRIKA**

Boit anasema hali hiyo imekuwa mbaya na kote ameshuhudia magari ya kuwabeba wagonjwa yenye mitungi ya hewa ya oksijeni.

Anakiri kuwapo mwanafunzi wenzake walioambukizwa virusi vya corona na katika kujihami, wamebuni mbadala wa kukutana kupitia makundi ya 'whatsapp' kuwawezesha kuwasiliana, pasipo kukutana.

Pia, ana simulizi binafsi aliposhuhudia uhalisia wa magari ya kwabeba wagonjwa mtaani yakiwa na mitungi ya hewa ya oksijeni.

Kiongozi huyo, anasema amekuwa akitumia usafiri wa pikipiki yake kufuatilia jinsi hali ilivyo katika hospitali mbalimbali katika maeneo ambako wapo Wakenya na Waafrika Mashariki wengine.

Sura ya mafanikio anayojinadi nayo, ni kwamba wanafunzi wenzake wamefaulu kujiandikisha mitandaoni, ili kuujulisha ubalozi wa Kenya usahihi wa waliko na hali zao.

**MAZITO KWINGINE?**

Denis Monda anasomea katika Chuo Kikuu cha Davangere, katika jimbo la Karnataka alikodumu kwa miaka minne, analalamika kuwapo ubaguzi wa rangi hasa weusi wanapopelekwa hospitalini na hawapewi kipaumbele

Anasema, kwa sasa jimboni aliko kumetangazwa marufuku ya kutotoka na hali imekuwa ngumu kwa raia wote wa kigeni, ambao sasa wamelazimika kuchukua tahadhari za kujihami.

Monda ana simulizi ya hatua alizochukua, kwa kuwasilisha namba yake ya mawasiliano kwa ubalozi wa Kenya, ili kufungua mawasiliano na wanafunzi wenzake walioko India.

Ubalozi wa Kenya nchini India, umewataka Wakenya walioko nchini humo kujiandikisha na kujiunga na makundi ya mawasiliano ya 'whatsapp' ili kuwasiliana kwa haraka panapotokea jambo la dharura.

**Kwa mujibu wa taarifa za mtandaoni.**

# Ugonjwa wa ubongo kwa watoto wenye madhila haya, wakinyimwa fursa shule

**INATOKA UK.12**

kuangalia. Kile unachokifanya mara kwa mara anajifunza na mpaka sasa ninaweza kumuachia mtu akaenda naye kwenye ibada," anasema.

**WATAALAMU WANENA**

Mtaalamu wa Elimu Jumuishi Kwenye Mfumo wa Kuwasaidia Watoto Wenye Usonji Katika Mazingira ya Shule jumuishi, Mariam Elisha, anasema ugumu unaojitokeza ni uwezo duni wa walimu kufundisha darasa jumuishi, wanashindwa kuelewa matatizo ya wenye usonji.

"Ili ufanye elimu jumuishi, mtoto mwenye usonji inatakiwa darasa lisizidi wanafunzi 20, lakini ndani ya darasa kuwe na mwalimu mwenye uelewa wa usonji, ambaye atasaidiana na mwalimu mwingine," anaelimisha.

Mwalimu kutoka Shule ya Msimbazi Mseto katika Kituo cha Usonji, Rukia Mohammed, anataja matatizo wanayokumbana nayo ni wako wachache wenye stadi hiyo, jumla yao wanne.

"Inapotokea tunampeleka mtoto mwenye usonji kwenye madarasa ya kawaida ili wachangamane na wenzao wajifunze, baadhi ya walimu husema hawawezi," anasema.

Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya Lukiza Autism Foundation (LUKIZA), Hilda Nkabe, inayojihusisha na usonji iliyoandaa maadhimisho hayo, anasema ana mtoto wa miaka 15, umri wa kuendelea na sekondari, amekosa pa kumwendeleza.

Daktari wa Watoto Mshauri wa Magonjwa ya Mfumo wa Fahamu na Ubongo kutoka Hospitali ya Saifee, ya Dar es Salaam, Yusuf Jamnagerwalla anawataka wadau kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, wakiliangalia kwa mapana, kwa sababu wanakua na baadae watahitaji kujitegemea.

**KUTOKA SERIKALINI**

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Daktari Godwin Mollel, anawaelekeza wataalamu ndani ya wizara, kuhakikisha zinapatikana takwimu sahisi za watoto wa kadi hiyo.

Dk. Mollel aliyeambatana na wataalam wa afya, anarejea takwimu za mwaka 2018, walikuwapo wanafunzi 1416 wenye usonji nchini.

Anahoji watoto hao kuonekana kuanzia wanapozaliwa, kliniki na ukuaji, lakini kuna uhaba wa takwimu. Hadi sasa, takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwapo walimu 157 katika shule 18 za msingi zenye watoto wenye usonji.

Pia kitaifa, takwimu za mwaka jana duniani, zinataja kuwapo wastani wa mtoto mmoja mwenye tatizo hilo, kutoka ndani ya kundi la watoto 132.

AFYA

# Unajua namna moyo mkubwa unavyouweka mwili shakani?

Na Christina Mwakangale

MOYO ni kiungo muhimu kwenye mwili wa binadamu na kitaalamu, inaelezwa katika viungo vinavyofanya kazi, ni cha kwanza kuumbwa tumboni mwa mama.

Kazi kuu ya moyo ni kusukuma damu safi katika viungo mbalimbali mwilini, pia kusafirisha hewa safi ya oksijeni.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Hospitali ya Heameda ya jijini Dar es Salaam, Dk. Hery Mwandolela, anasema uimara wa mwili na mfumo wa mishipa ya damu na moyo ni agalizo muhimu.

Anasema ili moyo ufanye kazi vizuri ni lazima uwe na uwezo na ukubwa unaokubalika kitaalamu, katika kufanya kazi ya kusukuma na kupokea damu vizuri

Dk. Mwandolela anasema, kuna magonjwa mbalimbali, ikiwamo mishipa ya damu inayochangia moyo kutanuka na kupoteza uwezo wake wa kusukuma na kupokea damu.

Mtaaluma huyo, anataja vyanzo vingine vya moyo mkubwa zaidi kuliko mahitaji, akiyaweka katika makundi ya: Mtoto kuzaliwa na tatizo la moyo, magonjwa ya moyo ambayo mtu anayapata ukubwani, uwiano usio sawa wa vichocheo, ujauzito na mengine ambayo vyanzo vyake havifahamiki.

Ingawa, Dk. Mwandolela anasema kundi kubwa la wanaoathiriwa na tatizo hilo la moyo kwa asilimia kubwa ni kutokana na magonjwa ya ukubwani, ikiwamo shinikizo la damu.




Bingwa wa Tiba ya Magonjwa ya Moyo, wa jijini Dar es Salaam, Dk. Hery Mwandolela, **PICHA: MTANDAO**

### SHIDA YA UZAZI

Dk. Mwandolela anasema, sababu ya moyo kuwa mkubwa huweza kuanza tangu mtoto akiwa tumbo ndani ya siku chache tangu mimba kutungwa na kwa kiasi kikubwa anasema kinachangiwa na hitilafu katika hatua kiumbe kinapojiunda tumboni.

"Mbegu ya baba inapokutana na mbegu ya mama na kutungwa mtoto, katika viungo vyote mfumo wa moyo ndio wa kwanza kujitengeneza kuliko kiungo chochote.

"Moyo ndio kiungo cha kwanza ambacho huanza kufanya kazi kuliko kiungo chochote. Ni takribani siku 20 tu tangu yai kuungana na mbegu, moyo huanza kufanya kazi," anasema.

Dk. Mwandolela anaendelea: "Moyo ni kiungo cha kwanza katika maisha ya binadamu na mwisho wa binadamu."

Anasema, inapotokea hitilafu katika wiki tatu za awali moyo huathiriwa na kunakuwapo uwezekano wa mtoto kuwa na tatizo la moyo baada ya kuzaliwa.

"Moyo kupanuka au kuwa mkubwa ni tatizo ambalo huathiri utendaji wa mfumo wa usambazaji damu mwilini," anafafanua.

Daktari huyo bingwa wa moyo, anasema mtoto anapopata maambukizi ya bakteria au virusi akiwa tumboni mwa mama, humsababishia tatizo.

"Tunajua mtoto ni mtegemezi kwa mama akiwa tumboni, wakati wa hatua za kiumbe kutengenezwa. Anaweza akapata maambukizi kutoka kwa mama. Pia, mtoto huweza kuzaliwa na shida ya valvu zake za moyo akiwa tumboni," anasema Dk. Mwandolela.

### ILIVYO UKUBWANI

Dk. Mwandondela anasema, magonjwa ya ukubwani kwa watu wazima, husababisha moyo kutanuka na kuharibu mfumo wa utendaji kazi mwilini.

Anaieleza shinikizo la juu la damu linalotumika kwa kipimo cha mekyuri na kinasomwa kwa viwango maalum ambazo ni msukumo wa damu, kawaida huwa kati ya 140/90 au 120/80 kwa viwango vya milimita.

Bingwa huyo anasema, kiwango cha juu ambacho kipimo hicho hutumika kina uwezo wa kutambua msukumo wa juu, ulio wa hatari.

"Shinikizo la juu la damu kila mara ni sababu ya kwanza moyo kutanuka au kuwa mkubwa. Misuli inayozunguka, moyo huanza kuwa minene na moyo utafanya kazi ya msukumo mkubwa, itashindwa kuhimili na kisha misuli ya moyo kuwa dhaifu," anabainisha Dk. Mwandolela.

Pia, anasema uchunguzi wa kubaini iwapo moyo una tatizo, hufanyika vipimo kadhaa kubaini ukubwa wa vyumba vya moyo.

Anasema, sababu zozote za moyo kutanuka au kuwa mkubwa bila kupatiwa tiba, zinachangia moyo kufeli.

Daktari huyo anafafanua kwamba yapo maambukizi ya magonjwa yanayoathiri mwili, ikiwamo moyo, kwani maambukizi ya muda mrefu, yanasababisha moyo kutanuka na kufanya usukumaji damu kuwa mdogo au wa chini.

Anataja Virusi vya UKIMWI (VVU), inashambulia misuli ya moyo na kuufanya kuwa mkubwa, pamoja na tatizo la valvu zake.

Kadhalika, anawataja watu wazima wenye tatizo la moyo, nao huathiriwa na bakteria wanaoshambuliwa valvu zake tangu utotoni.

Pia, Daktari Mwandolela, anasema kuna watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 10, huugua magonjwa ya virusi na kufanya valvu za miili yao ikiwamo moyo kushindwa kufanya kazi vizuri.

"Tatizo la valvu kushindwa kufanya kazi, hutokana na bakteria ambao huingia kwa njia ya hewa na koo kupata maambukizi, bakteria hawa hutoa sumu, kushambulia sehemu mbalimbali, msuli wa moyo," anasema Dk. Mwandolela.

Kwa mujibu wa tabibu huyo bingwa katika eneo la moyo, sumu zinazobakia hushambulia valvu na kuacha makovu na kuharibu mfumo wake wa kufunguka na kujifunga, wakati damu inapoingia na kutoka kwenye moyo.

"Kama valvu ilitakiwa ziwe zinakutana na kuachia au kujifunga, huachia kutokana na makovu, damu haitapita inayotakiwa, moyo utatumia nguvu na kutanuka," anasema.

"Tatizo la valvu huwa ni katika umri wa miaka 15 hadi 20, itakumbukwa kuanzia miaka ya 1980 hadi 1990, kulikuwa na idadi kubwa ya watoto waliokwenda (hospitalini) India kufanyiwa upasuaji wa moyo, ilitokana na maambukizi yaliyoanzia kwenye koo hadi kuharibu valvu," anabainisha.

### UJAUZITO JE?

Anasema wakati wa ujauzito, mama hupata shinikizo la damu na kusababisha moyo kutanuka na Daktari Mwandolela, anasema ni aina ya athari ngumu kuonekana mapema, mara nyingi hugundulika miezi mitatu ya mwisho ya ujauzito.

Dalili zake ni moyo kutanuka, unaenda kasi, damu inapungua mwilini, kuishiwa nguvu, miguu kuvimba na inachukua miezi mitano kuisha baada ya kujifungua.

"Ni ngumu kuutambua, hivyo mama mjamzito ni vizuri kuwahi katika kituo cha afya, ili kujua ni tatizo la moyo au la, inaweza kutibika kama ni mapema," anasema.

### VICHOCHEO MWILINI

Dk. Mwandolela ana ufafanuzi katika hilo, akisema: "Vichocheo ambavyo hutolewa katika maeneo tofauti ya mwili mfano, taifodi ambayo ipo sehemu ya shingoni, hutoa vichocheo kwa mizania sawa, ikiwa tofauti, huathiri moyo,"

Bingwa huyo wa tiba ya moyo, anashauri kwamba walio na dalili tofauti zikiwamo kuchoka kupita kawaida, moyo kwenda kasi, maumivu wa kifua, kikohozi wakati wa kulala, kizunguzungu, ni vyema wakafayiwa uchunguzi wa kitabibu kutambua mapema yanayojiri.



# Wakurugenzi h/mashauri kupimwa ufanisi fedha za lishe ya watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema itapima ufanisi wa wakurugenzi wa halmashauri katika kutenga Sh.1, 000 kwa kila mtoto kwa ajili ya lishe.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa maofisa lishe ambao unalenga kujadili uratibu na utekelezaji wa afua za lishe kwa ngazi ya mikoa na halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Prof. Shemdoe alisema pamoja na vipimo vingine vya ufanisi vinavyotumika kuwapima wakurugenzi hao, lakini pia suala la lishe ni kipimo kingine kwao.

Alisema kumekuwa na ongezeko la bajeti katika mamlaka za serikali za mitaa kutoka Sh. bilioni 11.6 mwaka 2017/2018 hadi kufikia Sh.bilioni 16.87, lakini kumekuwa na utoaji wa fedha za afua za lishe ambao si wa kuridhisha.

Aidha, aliwataka wadau wanaoshiriki katika afua za lishe kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa wanapotekeleza miradi yao na kutoa taarifa kila robo mwaka.

"Tukifanya hivyo kutasaidia kuepuka kupeleka fedha eneo moja na kufanya shughuli zile zile, bado kuna wadau wanafanya shughuli za lishe bila kuzingatia mkataba waliowekeana na uongozi, mashirika yasiyo ya serikali yanayofanya shughuli za lishe wahakikishe wanashirikiana na TAMISEMI,"alisema.

Naye, Mratibu wa Lishe, TAMISEMI, Mwita Waibe, alisema tangu kuanzisha idara katika mamlaka za serikali za mitaa pamoja na mambo mengine wameanzisha mfumo ambao unafuatilia na kupata taarifa sahihi za afua za lishe.

Mwita alisema sekta ya lishe inachangamoto ya watumishi kwani katika mikoa 26 ni mikoa 20 tu yenye wataalamu wa lishe na kati ya halmashauri 184 ni halmashauri 66 pekee zenye wataalamu hao.

"Hata kwenye halmashauri zienye wataalamu bado kuna mtu mmoja ni kazi ngumu kwani tumegatua masuala ya lishe katika ngazi ya vijiji na kata,"alisema.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki 80 wa mkutano huo, Mwenyekiti wa Maofisa Lishe, Bertha Donald, aliomba serikali kuhimiza utoaji wa fedha zilizitengwa kwa ajili ya lishe katika halmashauri.

"Kama tulivyomsikia kiongozi wetu (Waziri Ummy Mwalimu), alisema halmashauri ambazo hazijafikia asilimia 50 ya ukusanyaji mapato hawatoshi, na pia itumike kwa fedha zinazotolewa kwa kwa ajili ya lishe, kwani fedha zinatengwa lakini utoaji wa fedha hizo ni mgumu," alisema.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo juzi, kuhusu pikipiki zilizokamatwa na Jeshi hilo kwa tuhuma za kuhusika kufanyia uhalifu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wawekezaji kutoka Sweden waonyeshwa fursa kuwekeza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa wito kwa wawekezaji kutoka Sweden kuwekeza Tanzania kwa kuwa ina fursa na rasilimali nyingi kwa ajili ya biashara na uwekezaji.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alitoa rai hiyo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa kibiashara na uwekezaji katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sweden uliofanyika kwa njia ya mtandao, jijini hapa.

Alisema kuwa Tanzania kuna hali ya hewa na mazingira mazuri kwa ajili ya biashara na uwekezaji.

"Tanzania itaendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali ya Sweden na itaendelea kutekeleza makubaliano mbalimbali ya ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizi," alisema.

Waziri huyo alisema Tanzania inafanya jitihada mbalimbali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwamo sera na sheria kupitia utekelezaji wa "Blueprint", miundombinu ya usafirishaji nchi kavu, baharini na angani pamoja na kulifanya jiji la Dar es Salaam kuwa jiji kubwa la kibiashara ifikapo mwaka 2025.

"Nawasihi wawekezaji kuja kuwekeza nchini, ili kuiwezesha Tanzania kuuza mazao yaliyoongezwa thamani na si malighafi, pamoja na kubadilishana teknolojia ya kisasa kati ya Tanzania na Sweden," alisema.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Masuala ya nchi za Nordic wa Sweden; Waziri wa Ustawi wa Viwanda, Biashara na Ujasiriamali wa Kenya; Waziri wa TEHAMA na Ubunifu wa Rwanda na Waziri wa Biashara, Viwanda na Ushirika wa Uganda.

Wengine ni Balozi wa Tanzania nchini Sweden; Balozi wa Rwanda nchini Sweden na Naibu Kiongozi wa Mabalozi wa Afrika Mashariki nchini Sweden.

# Tulia apigia debe maendeleo ya Mbeya, Songwe

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Spika, Dk.Tulia Ackson, amewataka watu wanaotoka kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe wanaoishi Dodoma, kusaidia kuchochea maendeleo ya mikoa hiyo.

Akizindua Umoja wa Watu wa Mbeya na Songwe (UWAMBESO-Dodoma), jijini hapa, Dk.Tulia alisema suala la maendeleo ya mikoa hiyo ni jambo muhimu na wanapaswa kulizingatia.

Alisema wabunge wapo tayari kushirikiana nao katika kuhakikisha mambo wanayopanga yanafanikiwa.

"Tunataka maendeleo yafike kule, wale watu walivyotuchangua sisi kuja Dodoma ni ili tuje tuwasemee, lakini kusema ni jambo moja na kufanyika kule ulikotoka ni jambo la pili, na baadhi yenu hapa ni sehemu ya watu wanaoweza kusukuma haya mambo."

"Kwa hiyo moja wapo natamani UWAMBESO Dodoma iwe inafanya ni kutuletea wabunge mawazo yenu kuhusu maendeleo ya kule nyumbani, tushauriane humu ndani, tunaweza kuwa na wajenzi, wachora ramani,"alisema.

Aliwahimiza kuhakikisha wanaendeleza vijiji walivyotoka kwa kujenga nyumba bora nyumbani na kuwataka kuwa mfano wa kupeleka maendeleo kwenye maeneo yao.

"Tunaweza kujenga mjini na wakati wa kusindikizana ikawa mitihani, UWAMBESO tuwe sehemu ya kushauriana sio tukishasindikizana wakati wa kurudi ni mjadala wa kukosekana kwa choo, wewe peleka mjengo wako sasa tuachie wabunge tukusemee barabara ya kufika hapo, yale ya kutekelezwa na serikali tuleteeni tutayasemea,"alisema.

Naibu Spika huyo alipongeza kwa kuanzishwa umoja huo na kueleza kuwa utakuwa na tija katika kukuza uchumi.

Alitoa wito kwa viongozi kuhakikisha wanaongeza wigo wa wanachama kutoka katika wilaya zote za mkoa huo.

Naye, Katibu wa umoja huo, Baleke Mwakanosya, alisema umoja huo una wanachama takribani 140 ikiwa na malengo ya kushirikiana kwenye raha na shida.

Aidha, alisema umoja huo una mikakati ya kuwainua wanachama kiuchumi kwa kuanzisha chama cha kuweka na kukopa (SACCOS).

**"Kwa hiyo moja wapo natamani UWAMBESO Dodoma iwe inafanya ni kutuletea wabunge mawazo yenu kuhusu maendeleo ya kule nyumbani, tushauriane humu ndani, tunaweza kuwa na wajenzi, wachora ramani,"alisema.**





# Wakutwa wamekufa, kutumbukizwa mtoni

**Na Grace Mwakalinga ,**
MBARALI

WATU watatu wa jamii ya wafugaji wamekutwa wameuawa na miili yao kutupwa ndani ya maji katika Mto Ruaha Mkuu kwenye ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, huku watu wengine watatu ambao wanadaiwa walikuwa wakichunga mifugo pamoja na marehemu hao hawajulikani walipo. Tukio hilo la mauaji linadaiwa kutokea April 26, mwaka huu, katika Bonde la Ihefu lililoko ndani ya Hifadhi ya Raifa ya Ruaha wilayani Mbarali.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Matagri Mbigili, alisema watu hao waliouawa ni wa jamii ya wafugaji wanaoishi Kijiji cha Magwalisi, Kata ya Igava wilayani hapa.

Alisema baada ya kupata taarifa za mauaji hayo, alitoa taarifa kwenye vyombo vya dola na kuongozana na timu ya vyombo vya ulinzi na usalama kwenda kusaka miili ya marehemu ndani ya hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mbigili alisema katika timu hiyo waliongozana na askari wa Polisi, daktari na askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Walipofika ndani ya Bonde la Ihefu, alisema walipata miili ya watu wawili ikiwa imetupwa ndani ya Mto Ruaha Mkuu pamoja na kichwa cha mtu mwingine kikiwa hakina kiwiliwili.

Alisema daktari waliyeongozana naye, alifanya uchunguzi wa kitabibu kuhusu chanzo cha vifo hivyo na akasema kuwa watu hao waliuawa.

"Daktari alisema kichwa cha mtu tulichokipata kilikuwa na jeraha la kuchomwa na kitu chenye ncha kali kilichoingilia chini ya sikio la kushoto na kutokea upande wa kulia wa kichwa, hali ambayo inaonyesha kuwa waliuawa," alisema.

Kaka wa mmoja wa marehemu, aliyejitambulisha kwa jina la Mbuga Salawa, alisema mdogo wake aliondoka nyumbani na wenzake kwenda kuchunga ndama.

Alisema wakiwa wanachunga mifugo yao, walikurupushwa na askari wa TANAPA ambao waliwafukuza na kuwakamata baadhi yao. Wale waliofanikiwa kuwakimbia askari hao, alisema ndio walitoa taarifa za kukamatwa kwa wenzao na ndipo wakaamua kufuatilia katika ofisi za TANAPA za Ikoga.

"Tulipofika kwenye kituo cha TANAPA, hatukumkuta ndugu yetu na ndipo tukaongozana na askari kwenda hifadhini ambako tulifanikiwa kupata kichwa chake kikiwa ndani ya maji ya Mto Ruaha," alisema Salawa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Makresia Pawa, alisema hayo ni mauaji ya 12 yaliyotokea ndani ya miaka miwili, yote yakituhumiwa kufanywa na askari wa TANAPA.

Pawa aliiomba serikali kuweka alama ya mipaka ya hifadhi ya taifa dhidi ya maeneo ya wananchi ili kuepusha migongano baina ya hifadhi na wananchi pamoja na mauaji ya mara kwa mara.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuwa watulivu wakati huu ambao vyombo vya dola vinaendelea kushughulikia suala hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, amethibitisha kutokea kwa vifo hivyo.

Matei alisema taarifa zilizopo ni kwamba watu waliokuwa ndani ya hifadhi hiyo walikuwa sita na tayari jeshi hilo limepata miili ya watu wawili na kichwa cha mtu mmoja huku wengine watatu wakiwa hawajulikani waliko.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuwasaka watu ambao hawajulikani waliko pamoja na kutafuta chanzo cha mauaji pamoja na watu wanaodaiwa kuhusika na mauaji hayo.



Baadhi ya wanafunzi Shule ya Sekondari Mwale, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakipokea viti 100 na meza 100, vilivyotolewa na Mbunge wa Jimbo hilo, Francis Mtega kupitia mfuko wa jimbo, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Shule yakosa mawasiliano ya barabara kutokana na mvua

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

SHULE ya Sekondari Muale iliyoko Kata ya Chimala wilayani Mbarali haina mawasiliano ya barabara kutokana na barabara pekee inayoingia shuleni hapo kukatika kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chimala, Sophia Menda, alisema jana kuwa kutokana na kuharibika kwa barabara hiyo, kwa sasa gari pekee linaloweza kufika shuleni hapo ni trekta kwa vile lina uwezo wa kupita katika barabara mbovu.

Alisema shule hiyo ni mpya ambayo bado ujenzi wake unaendelea na kwamba tangu ianzishwe miaka mitatu iliyopita, hakuna barabara rasmi iliyowahi kujengwa kuingia shuleni hapo.

"Tumekuwa tukitumia barabara ya asili ambayo kwa sasa imekatika kabisa kutokana na mvua, hali hii inasababisha gari pekee linaloweza kufika hapa kwa sasa kuwa trekta," alisema Menda.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba halmashauri ya wilaya kusaidia kufungua mawasiliano ya barabara shuleni hapo ili kurahisisha shughuli mbalimbali zinazohusu maendeleo kufanyika. "Bado tunaendeleoa na ujenzi wa shule yetu lakini katika kipindi kama hiki hatuwezi kuingiza vifaa vya ujenzi au hata vifaa vingine kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi kutokana na ubovu wa barabara, hivyo tunaiomba serikali yetu itusaidie katika hili," alisema.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema kwa sasa wanayo matatizo mengi ambayo yanahitaji ufumbuzi ili waweze kujisomea katika mazingira rafiki.

Mmoja wa wanafunzi hao, Geofrey Wilfred, alisema kwa sasa shuleni hapo wana uhaba wa vitabu vya kiada na ziada, hawana vyumba vya madarasa vya kutosha, uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi, maabara na ukosefu wa viwanja vya michezo.

Akizungumzia matatizo ya shule hiyo, Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, alisema changamoto zinazoikabili shule hiyo ni nyingi lakini ufumbuzi wake umegawanyika katika makundi matatu.

Alisema yako matatizo ya kisera ambayo yanaweza kupatiwa ufumbuzi na serikali Kuu, tatizo la miundombinu ambalo linawagusa moja kwa moja wananchi na halmashauri yao na zile ambazo zinapaswa kushughulikiwa na uongozi wa kijiji.

Mtega alisema matatizo yote hayo anayachukua kwa lengo la kuyafikisha mahali husika na zile ambazo ziko ndani ya uwezo wake atajaribu kutatua yeye mwenyewe.

# Mbeya yapewa bil. 4.5/- ujenzi wa hospitali tatu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya ilipokea zaidi ya Sh. bilioni 4.5 katika mwaka wa fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya katika halmashauri tatu ambazo zilikuwa hazina hospitali za hadhi hiyo.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Salum Manyata, alisema hayo jana alipokuwa anazungumza na gazeti hili kuhusiana na maendeleo ya sekta ya afya katika mkoa.

Alisema fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizo katika halmashauri za Mbeya, Mbarali na Busokelo. Alisema kila halmashauri ilipatiwa mgawo wa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba kila moja.

Pia alisema katika mwaka wa fedha wa 2019/20 walipokea Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hizo pamoja na kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya Jiji la Mbeya.

Vilevile alisema Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipokea zaidi ya Sh. milioni 400 kutoka katika Shirika la Global Fund kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Makandana pamoja na ujenzi wa jengo la mama na mtoto.

"Mwaka wa Fedha 2020/21 Sh. bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali za halmashauri tatu ambazo kila halmashauri itatumia Sh. Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi na Sh. milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba," alisema Dk. Manyata.

Pia alisema mpaka sasa mkoa wa mbeya una vituo 352 vya kutolea huduma za afya ambavyo kati ya hivyo, zahanati ni 297, vituo vya afya 35 na hospitali 20.

**Pia alisema katika mwaka wa fedha wa 2019/20 walipokea Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hizo pamoja na kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya Jiji la Mbeya.**



# Waziri asisitiza umuhimu chanjo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wazazi na walezi kuwapatia watoto wao chanjo kwa kuwa ni kinga kubwa ya maradhi yanayozuilika.

Amesema chanjo ni muhimu kwa watoto katika kuimarisha makuzi yao na kuwafanya wawe na afya bora iwapo watapatiwa kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mazurui alieleza hayo jana, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Chanjo Afrika ambapo kwa Zanzibar ulifanyika katika Kituo cha afya cha Mwera, Mkoa wa Kusini Unguja. Kaulimbiu ya Wiki ya Chanjo Afrika kwa mwaka huu ni 'Chanjo Huweka Jamii Pamoja.'

Aliwataka wananchi wasipuuze kuwapeleka watoto wao katika vituo vya afya kupatiwa chanjo na kinga kwa kuwa ni bora na rahisi kuliko tiba.

Waziri wa Afya huyo aliikumbusha jamii kuwa lengo la Afrika kuweka wiki maalumu ya chanjo ni kuwatanabahisha umuhimu wake na kutoa fursa kwa watoto waliofika umri wa kupata chanjo kupatiwa na ambao hawajakamilisha na umri wao hauzidi miaka mitano wapelekwe vituoni kukamilisha.

Aidha, aliwashauri wazazi wa kiume kuwapa ushirikianao wenza wao katika kufanikisha mpango wa chanjo kwa watoto wao kwa sababu baadhi wameonekana kutowapa ushirikiano.

Naye Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Hadid Rashid Hadid, alisema wananchi wa mkoa huo wana mwamko mkubwa katika suala la chanjo na kwa mujibu wa takwimu wanaongoza kwa mikoa yote ya Tanzania.

Alimhakikisha waziri kwamba uongozi wa mkoa huo utaendelea kusimamia na kufanya kila juhudi ili kuhakikisha watoto wote wanapatiwa chanjo kwani ni moja kati ya haki yao ya msingi.

Hata hivyo, Hadid alikiri kuwa wapo kinamama wachache ambao hawakamilishi chanjo kwa watoto wao na mkakati wa kuwahimiza utawekwa ili wakamilishe na kuendelea kuwa mfano kwa mikoa mengine.

Kaimu Daktari Mdhamini Kituo cha Afya Mwera, Salma Bakari Muhd, alisema kituo hicho kimekuwa kikifanya vizuri katika kutoa chanjo za watoto ingawa bado kuna baadhi ya kinababa wamekosa mwamko na kuhisi kuwa kazi ya kuwapeleka watoto vituo cha afya ni kazi ya kinamama.

# Serikali yaanza uhakiki wa wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, amesema serikali ya mkoa huo imedhamiria kufanya uhakiki wa wafanyakazi wa Manispaa ya Mjini hususani wa vitengo vya usafi ili kuona uhalali wao.

Idrissa alisema hayo jana katika kikao maalumu cha wafanyakazi wa manispaa ya Mjini kilichowashirikisha viongozi wa wilaya na manispaa hiyo kuhusu kukumbushana na kuhimizana wajibu wa utekelezaji wa majukumu.

Alisema pamoja na jitihada mbalimbali za kuhimiza na kusimamia uwajibikaji kwa watendaji wa manispaa katika suala la usafi, bado mafanikio yaliyopo si ya kuridhisha hatua ambayo inaleta shaka kwa wingi wa wafanyakazi waliopo na ufanisi wa kazi.

"Lazima tufanye uhakiki wa wafanyakazi wetu na kulipa mishahara. Hii itasaidia kujua kama kweli wapo au kuna wafanyakazi hewa maana Manispaa ya Mjini ina wafanyakazi wengi kulinganisha na manispaa zetu zingine katika mkoa huu. Lakini bado suala la usafi pia limekuwa likipigiwa kelele kila siku bila mafanikio," alisema Idrissa.

Aidha, Mkuu wa Mkoa huyo aliuagiza uongozi wa Manispaa ya Mjini kuandaa utaratibu maalumu kwa wafanyakazi wa vitengo vya usafi ili kuona kama wanawajibika ipasavyo katika kufikia malengo ya serikali ya kuuweka mji katika mazingira mazuri.

Hata hivyo, aliwahakikishia wafanyakazi hao kuwa serikali ya mkoa itafanya kila iwezalo kuona inawatengenezea mazingira bora ya utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo ulipwaji wa stahiki zao kwa wakati hususani wafanyakazi wa mazingira magumu.

" Pamoja na kukuhimizeni kuhusu uwajibikaji katika nafasi zenu za kazi lakini pia tutahakikisha tunashuhulikia haki zenu mlipwe tena kwa wakati ili kuona sasa mnafanya kazi tukiwa tumewapunguzia kero ndogo ndogo," alisema.

Baadhi ya wafanyakazi wa Baraza la Manispaa ya Mjini, waliuomba uongozi wa serikali ya Mkoa kuwaondolea changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kuwapatia ruzuku na stahiki zao pamoja na huduma ya afya hususani wafanyakazi walio kwenye mazingira magumu wakiwamo wafagiaji na wasafisha michirizi.

"Tunaomba sana tusaidiwe, tumekuwa na vilio vya siku nyingi. Kila kiongozi anayekuja kwa awamu tofauti katika mkoa, wilaya na manispaa tumekuwa tukiwasilisha matatizo yetu lakini hayachukuliwi hatua hususani suala la stahiki kwa maana ya posho. Lakini pia huduma ya afya ikiwamo bima ya afya," alisema Juma Ali kwa niaba ya wafanyakazi wezake.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mjini, Suleiman Mohammed Rashid, aliuomba uongozi wa mkoa kushirikiana na wizara husika kuufanyia maboresho mfumo wa muundo wa manispaa ili utambulike katika idara ya utumishi.



Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Joanitha Mrengo (wa tatu kushoto), Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard (wa tatu kulia), Mkuu wa Biashara wa Benki hiyo upande wa Zanzibar, Abdallah Duchi, mwakilishi wa wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar, Anwar Haji (kulia), Mkuu wa Masoko wa Taasisi ya Aiesec Tanzania, Abdulkarim Bihaki (kushoto) na Rais wa taasisi hiyo, Michael Chacha (wa pili kushoto), wakionyesha ishara ya mshikamano baada ya mkutano na waandishi wa habari jana, kuhusu kongamano la wanafunzi wa vyuo vikuu litakalofanyika Zanzibar lililoandaliwa na Benki hiyo, kesho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yaelekeza nguvu ajira kwa vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imesema imedhamiria kusaidia vijana katika soko la ajira pamoja na kuibua vipaji kutoka vyuoni ambao vitakuwa na uwezo wa kukuza uchumi kupitia ajira.

Akizungumza jana katika mkutano na waandishi wa habari mjini hapa, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard, alisema benki hiyo imeandaa kongamano maalum katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa lengo la kuwakutanisha wanafunzi wa vyuo vikuu kuzungumza nao na kuwapa mbinu mbalimbali za ajira na kujiajiri.

"Mbali na huduma mbalimbali ambazo mwanafunzi anaweza kuzipata kupitia NMB, benki pia itamletea elimu maalumu ya masuala ya kifedha, elimu ya akaunti mbalimbali za NMB ambazo mwanafunzi anaweza kufungua na kujiandaa na maisha baada ya chuo," alisema Richard.

Alibainsha kuwa kongamano hilo litakaloanza leo linaitwa 'NMB Career Fair' maalum kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vikuu kushirikiana na benki ili kutambua fursa mbalimbali ambazo mwanafunzi anaweza kuzipata kupitia benki hiyo akiwa mwanafunzi na hata akishamaliza chuo.

Pia alisema NMB ina programu nyingi zinazompa nafasi kijana kushiriki kama mfanyakazi, mwanafunzi aliye kwenye mafunzo na pia kuwapa uzoefu wa kazi ili kukidhi vigezo vya uzoefu kazini, hivyo kufanikiwa vyema kwenye soko la ajira.

"Tuna programu maarufu inayong'amua vipaji vya vijana wanaotoka vyuoni na kuwachukua kuja kufanya kazi kwetu. Program hii inaitwa 'Management Trainee' ambayo mwanafunzi anayechukuliwa anawekwa kwenye uangalizi na kufundishwa mambo mbalimbali na baada ya miaka miwili kama atafanikiwa anapata ajira. Kwa miaka mitano iliyopita, zaidi ya vijana 50 wameshanufaika na programu hii," alisisitiza Richard.

Mkuu wa Rasilimali Watu NMB, Joanitha Rwegasira, alisema: "Kwa tukio la leo tunategemea kukutana na zaidi ya wanafunzi 1,000 wanaotoka vyuo vikuu zaidi ya 10 vya Zanzibar.

Alisema watakaohudhuria wataondoka na zawadi mbalimbali na pia watapata elimu nzuri ambayo pengine wasingeipata sehemu nyingine yoyote.

"Sisi kwetu vyuo vikuu ndipo sehemu ambapo tunatoa wataalam wetu na kupitia makongamano kama haya. Pia tunaangalia vipaji ambavyo tutaweza kufanya navyo kazi huko mbeleni," alisema Rwegasira.

Rais wa Wakala wa Ajira Tanzania (AISEC), Michael Chacha, alisema makongamano ya namna hiyo yanawasaidia wanafunzi kujitambua lakini pia kutengeneza fursa za ajira na pengine kujiajiri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA ZINAUZWA

**NYUMBA TATU ZINAUZWA KWA PAMOJA KWA MTOGOLE ZIPO BARABARANI VYUMBA 11 NA MADUKA MATATU,MILLIONI 150**

**KWA MAWASILIANO:0716 150 251**

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO. 107/2021**

Ombi la **MARTHA MHINA MACHUPA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MOHAMED HASSAN BAGULE** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 27/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.


**Tarehe 15/04/2021**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STANLEY F KISAMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLA** yenye namba za usajili **T 741 AFY** ,Yyeyote atakayeikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/TAB/R-B/218714/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PRIVATUS ADRIANO NDYALI** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **S.3501/00601** kilichotolewa na **HOPE SEKONDARI** mwaka **2014**. Cheti cha Chuo chenye namba **19312** kilichotolewa na **MARANGU TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/RUH/RB/46961/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi No.113/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ISAYA PETRO MBOGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAMSON ISAYA MBOGO**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5 (2)ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/Maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 12/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu unaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 27/4/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEJERI ATHUMANI GILLAH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 963 DEB.**Chassis **No.DO61T219944**,Engine **No.F6AJAAIO10479.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/-DOD/RB/211130/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **DAUDI BUSOKA MAKEBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari Yenye namba za usajili **T – 863 DVZ** yenye Chassis namba **ACU100012206 TOYOTA HARIER OLD MODEL.** Kwa atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa Kumb: **MWA/NY/R-B/219032/2021**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

PHILBERT EXUSPER NEMES ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA COROLLA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 542 CKH NA CHASSIS NO. NZE 1213246550 NA ENGINE NO. INZB093876 TAARIFA YA POLISI KAH/ TR /RB/ 2500/2018

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.03.2021

Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Mar-21 | Robo Mwaka ya 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4 929 | 3 157 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 6 458 | 4 715 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 29 966 | 24 005 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4 285 | - |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 14 525 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 32 006 | 61 199 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 67 846 | 55 963 |
| 12 | Mali Nyingine | 7 615 | 5 957 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1 334 | 1 978 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **154 439** | **171 500** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 36 970 | 23 878 |
| 18 | Amana za Wateja | 75 781 | 105 050 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 9 020 | 8 203 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 917 | 19 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2 829 | 7 271 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3 725 | 3 608 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **129 242** | **148 029** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **25 197** | **23 471** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31 420 | 31 420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29 104 | 29 104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (37 053) | (40 498) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1 727 | 3 445 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25 197** | **23 471** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 869 874 | 860 148 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3 873 | 4 102 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 390 | 225 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 14% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.19% | 7.33% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74% | 49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 44% | 33% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84% | 82% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -25% | -5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -10% | -24% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31 420 | 29 104 | (37 053) | - | - | - | 23 471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1 727 | - | - | - | 1 727 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31 420** | **29 104** | **(35 327)** | **-** | **-** | **-** | **25 197** |
| **Mwaka uliopita 2020** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31 420 | 29 104 | (40 498) | - | - | - | 20 026 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3 445 | - | - | - | 3 445 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31 420** | **29 104** | **(37 053)** | **-** | **-** | **-** | **23 471** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-21 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2 803 | 2 578 | 2 803 | 3 958 |
| 2 | Gharama za Riba | (765) | (646) | (765) | (1 510) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2 038** | **1 933** | **2 038** | **2 447** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3 068** | **4 340** | **3 068** | **2 323** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 312 | 471 | 312 | 307 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 2 719 | 3 854 | 2 719 | 1 998 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 38 | 16 | 38 | 18 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3 352)** | **(3 785)** | **(3 352)** | **(3 749)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1 615) | (1 701) | (1 615) | (1 794) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (305) | (299) | (305) | (296) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1 431) | (1 785) | (1 431) | (1 659) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1 754** | **2 488** | **1 754** | **1 021** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (28) | (62) | (28) | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1 727** | **2 426** | **1 727** | **1 021** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1 727** | **2 426** | **1 727** | **1 021** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 114 | 114 | 114 | 117 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 275 | 386 | 275 | 163 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.06% | 1.42% | 1.06% | 0.46% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.10% | 8.90% | 7.10% | 4.98% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 57.09% | 54.71% | 57.09% | 59.69% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.50% | 1.41% | 1.50% | 1.25% |

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Kingsley Ulinfun<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | *Imesainiwa* | *28th April 2021* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *28th April 2021* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *28th April 2021* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *28th April 2021* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *28th April 2021* |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Mar-21 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1 754** | **2 488** | **1 754** | **1 021** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 133 | 501 | 133 | 128 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (11 883) | (8 571) | (11 883) | (1 722) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | (2) | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (15 361) | 47 476 | (15 361) | (1 953) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (5 960) | (84) | (5 960) | (2 225) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 117 | (66) | 117 | (3 581) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1 657) | (858) | (1 657) | 3 486 |
| - Kodi Iliyolipwa | (28) | (62) | (28) | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(32 885)** | **40 823** | **(32 885)** | **(4 845)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (51) | (296) | (51) | (36) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 5 | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(51)** | **(290)** | **(51)** | **(36)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | (3 510) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **(3 510)** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(32 936)** | **40 533** | **(32 936)** | **(8 390)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 119 074 | 78 542 | 119 074 | 116 710 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **86 138** | **119 074** | **86 138** | **108 320** |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

UBA Africa's global bank

HABARI MICHEZO



# Fernandes afikiria ukocha Man United

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amesema anatarajia kuhamia kwenye kazi ya ukocha pindi atakapotundika daluga, na na matumaini yake ni kuiongoza Manchester United hapo baadaye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ureno, amefanikiwa kuwa na mwanzo mzuri hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Tayari ameweka malengo yake hayo ya muda mrefu na amesema angependa kukaribisha fursa hiyo kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England mara atakapostaafu kucheza soka.

Fernandes alisema hayo wakati wa maswali na majibu kwenye tovuti rasmi ya United juu ya azma yake ya kufundisha: "Sasa naona wakati unapita na kuona watoto wakitoka 2000, 2001, 2002, na dada yangu anatoka 2000, kwa hiyo inaleta mkanganyiko kichwani mwangu.

"Ninajaribu kufurahia mpira wa miguu, unajua. Nadhani nataka kuwa kocha. Kwa kweli, ningependa kuwa mkufunzi.

"Sijui ni timu gani ningependa kusimamia. Kwa kweli, timu kubwa ikiwa nitaweza kuisimamia Manchester United, nitafurahi."



# Benzema atuliza presha ya Zidane kwa Chelsea

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amemsifia Karim Benzema, lakini amesisitiza hashangazwi na kiwango cha kufunga mabao kwa mshambuliaji huyo, wakati 'Los Blancos' hao wakilazimishwa sare ya bao 1-1 na Chelsea kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Benzema aliisawazishia Madrid juzi Jumanne – wakati Mfaransa huyo akifuta bao la Christian Pulisic la dakika ya 14 kwenye mchezo huo uliopigwa jijini Madrid.

Benzema aliifikia rekodi ya Raul aliyepo nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji wanaoongoza kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akifikisha bao lake la 71.

Ni Lionel Messi (36) na Cristiano Ronaldo (35) pekee ndio wamefunga mabao mengi zaidi dhidi ya timu tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Benzema akifikisha 33, sawa pa na Raul.

Benzema, pia alifikisha bao la sita msimu huu kwenye mashindano hayo.

"Karim ni mchezaji wa aina yake nina furaha kuwa naye, lakini sishangazwi kwa kile anachofanya katika kila mchezo," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Hali ni sawa kwa wachezaji wangu wote. Wote ni muhimu sana kwangu, wamefanya kazi ya ziada kwenye mchezo wa leo (juzi).

"Nina furaha kwa wachezaji wote. Tunajua kwamba tunakwenda London na tunatakiwa kufunga mabao ili tuweze kufuzu fainali."



# Navas ajifunga PSG hadi 2024

**PARIS,** Ufaransa

KIPA namba moja wa timu ya PSG, Keylor Navas, ameongeza mkataba wa mwaka mmoja wa kuendelea kucheza hapo hadi mwaka 2024.

Navas alihamia PSG akitokea Real Madrid mwaka 2019, na tangu atue PSG amekuwa muhimili muhimu sana wa timu hiyo.

Navas amecheza mechi 72 klabuni hapo na amesaidia timu yake kunyakua Kombe la Ligue 1, Coupe de France na Coupe de la Ligue msimu uliopita.

Baada ya kusaini mkataba huo, Rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi, alieleza kufurahishwa na kitendo hicho kwani ni mmoja wa wachezaji bora kabisa.

"Nimefurahishwa sana na Navas kuongeza mkataba wake, ni mchezaji mzuri na anajiamini uwanjani na kupendwa na mashabiki," alisema Nasser akiwaambia waandishi wa habari.

PSG sasa wapo katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na jana usiku walicheza mchezo wao wa kwanza dhidi ya Manchester City.



# Bayern yamchukua Nagelsmann rasmi

**MUNICH,** Ujerumani

JULIAN Nagelsmann anatarajiwa kuwa kocha mkuu wa Bayern Munich baada ya Hans Flick kuomba kuachana na klabu hiyo na amekubali dili la mkataba wa miaka mitano, ambao utaanza Julai Mosi, klabu hiyo ya Bundesliga imethibitisha.

Bayern ambao wapo karibu kushinda ubingwa wa tisa mfululizo wa Bundesliga, wamekubali kukatisha mkataba na Flick, ambaye aliitaarifu klabu kuwa hataendelea kuwa kocha mkuu baada ya msimu huu.

"Julian Nagelsmann anawakilisha kizazi kipya cha makocha," Rais wa Bayern, Herbert Hainer alinukuliwa na vyombo vya habari vya Ujerumani katika maelezo yake.

"Licha ya umri wake mdogo, lakini amekuwa na ushawishi katika kazi yake hiyo. Tumeshawishika kwa pamoja na Julian Nagelsmann tutajijenga kupata mafanikio makubwa ambayo tumepata katika miaka michache iliyopita."

Mazungumzo yalizuka Jumatatu kwamba, Bayern na Nagelsmann walikuwa wamekubaliana haraka.

Kwa mujibu wa ripoti zilizoenea nchini Ujerumani na Ulaya, makubaliano yamefikiwa kati ya klabu hizo ambapo ingemfanya Nagelsmann kuwa kocha mkuu ghali zaidi duniani.

Taarifa zinaonyesha Bayern watalipa karibu euro milioni 20, wakati ripoti zaidi zinaonyesha pamoja na nyongeza anaweza kuchukua jumla ya karibu euro milioni 25.

Nagelsmann mwenye umri wa miaka 33, alikuwa pia akihusishwa na Tottenham Hotspur baada ya uamuzi wao wa kumtema Jose Mourinho wiki iliyopita.

# Real Madrid waigomea Arsenal kwa Odegaard




**MADRID,** Hispania

REAL hawatarajii kumuweka sokoni, Martin Odegaard katika dirisha lijalo la uhamisho kwa sababu wanatarajia kumtumia kwenye kikosi cha kwanza.

Nyota huyo aliungana na Arsenal kwa mkopo Januari mwaka huu kwa muda wa miezi sita, mkopo wake ni wa sita katika kipindi chake na Madrid.

Kocha Zinedine Zidane sasa anatarajia kumpa majukumu Odegaard kwenye kikosi chake cha kwanza kwa msimu wa 2021-22.

Arsenal wanaripotiwa kuwa walikuwa wanahitaji kumsaini staa huyu katika mkataba wa kudumu kwa miezi ijayo.

Lakini sasa jambo hilo litakuwa gumu kwa sababu ya mpango wa Real, vinginevyo kuwe na mabadiliko katika mipango yao juu ya staa huyu.

Kwa mujibu wa chanzo cha Diario AS, Zidane anajilaumu kumruhusu Odegaard kuondoka kwa mkopo klabuni hapo, kwa sababu alikuwa akipata shida kujaza nafasi za Luka Modrid na Toni Kroos wanapokuwa majeruhi.

# Pulisic: Mimi, Hazard ni tofauti kabisa

**MADRID**, Hispania

CHRISTIAN Pulisic amekataa kufananishwa kwake na mchezaji wa zamani wa Chelsea, Eden Hazard na kusisitiza kwamba, yeye anacheza kwa mtindo wake binafsi.

Pulisic alikuwa nyota kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baina ya Chelsea na Real Madrid kwa kufunga bao la uongozi, wakati timu hizo zikitoka sare ya kufungana bao 1-1, Jumanne.

Nyota huyo wa Marekani alitua pale Stamford Bridge akitokea Borussia Dortmund wakati wa majira ya joto mwaka 2019, muda mfupi baada ya kukamilika kwa dili yas Hazard kwenda Madrid.

Pulisic anajivunia sifa nyingi kama Hazard, ambaye aliona kama mfano wa kuigwa mapema wakati akianza soka, lakini kijana huyo mwenye umri wa miaka 22, ana hamu ya kujitengenezea sifa yake mwenyewe pale Chelsea badala ya kufuata nyayo za




Mbelgiji huyo.

Alipoulizwa kuhusu kufananana kati yake na Hazard, Pulisic aliuambia mkutano wa waandishi wa habari: "Alikuwa mchezaji mzuri katika klabu hii ya mpira wa miguu. Kwa kweli, nilikuwa nikimtazama. kujaribu kuwa kama yeye.

"Mimi nina uchezaji wangu mwenyewe, anayefanya bidii kwa klabu hii. Ni wazi, alikuwa mchezaji mkubwa kwa klabu hii na ni wazi ni heshima kusikia kulinganishwa kama hivyo, lakini bado nina njia yangu ya kucheza.

"Sipendelei kufananishwa na yeye kwa uchezaji, kwani mimi nina staili yangu binafsi ya kucheza.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AANDALIWA OFA NONO ISIYOPINGIKA PSG

**Haitafikiwa na klabu yoyote, wamepanga kumpa mkataba wa miaka miwili, lakini utakuwa na kipengele cha...**

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain inaandaa ofa "isiyopingika" kwa Lionel Messi ili kufanikisha uhamisho wake wa kutoka Barcelona, kwa mujibu wa ripoti ya TNT Sports.

Messi bado hajasaini mkataba mpya na Barcelona ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu na kumekuwa na uvumi mwingi kuhusu majaliwa ya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Na sasa PSG inajiandaa kutumia nafasi hiyo kwa kutoa ofa kubwa ambayo haitaweza kufikiwa na klabu yoyote ili kumsajili kipindi cha uhamisho wa majira ya joto kinachokuja.

**Kwa mujibu wa ripoti, miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, watatoa ofa ya mkataba wa miaka miwili kwa Messi, huku kukiwa na kipengele cha kumuongezea mwaka mmoja zaidi.**

"Ni ofa ambayo haitafikiwa na klabu yoyote," kilieleza chanzo kimoja kutoka ndani ya PSG kikinukuliwa na TNT Sport.

"Wamepanga kumpa mkataba wa miaka miwili, lakini utakuwa na kipengele cha kumuongezea mwaka mmoja zaidi na wana imani ofa hiyo haifafikiwa na yeyote."

Klabu hiyo inaamini kwamba, itaweza kumshawishi Messi kujiunga na PSG kwani atakuwa na nafasi ya kushinda mataji mengi zaidi akiwa hapo jijini Paris.

Messi bado hajaonyesha nia ya kutaka kusaini mkataba mpya na Barcelona, huku Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta akipambana kuhakikisha anambakiza klabuni hapo.

## KWA UFUPI

### WENGER KURUDI ARSENAL
KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, anajiandaa kujiunga na mpango wa kuinunua klabu hiyo pamoja bilionea Daniel Ek na wachezaji wake watatu wa zamani. **(BeIN Sports, via Mirror)**

### LIVER YAKOMAA NA KONATE
LIVERPOOL bado wana mpango wa kumsajili beki wa RB Leipzig, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21, kwa dau la pauni milioni 40 mwishoni mwa msimu, licha klabu hiyo kutangaza hasara ya pauni milioni 46. **(Mail)**

### FLICK KUMRITHI LOW
SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Ujerumani, linatarajiwa kuanza mazungumzo na kocha anayeondoka katika klabu ya Bayern Munich, Hansi Flick, ili kuchukua nafasi ya Joachim Low kama kocha wa timu ya taifa hilo. **(90min)**

### RODGERS HAENDI SPURS
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers hana mpango wa kuhamia Tottenham Hotspur kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Jose Mourinho aliyetimuliwa. **(Sky Sports)**

### LINGARD KUBAKI WEST HAM
WINGA wa timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 28, atapigania kuihama klabu ya Manchester United mwishoni mwa msimu huu, wakati mkataba wake wa mkopo na West Ham utakapomalizika. **(Eurosport)**

### AGUERO HUYO INTER
KLABU ya Inter Milan imeingia katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, ambaye ameshatangaza kuondoka Manchester City baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu. **(Caciomercato)**

### DAVID AWINDWA ARSENAL
MSHAMBULIAJI wa Lille, Jonathan David mwenye umri wa miaka 21 raia wa Canada, yupo katika mawindo ya Manchester United na Arsenal. **(Fichajes.net)**

### LEEDS YAMTAKA KVARATSKHELIA
LEEDS United wamefanya mazungumzo juu ya kumsajili winga wa klabu ya Rubin Kazan na raia wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 20. **(Football Fancast)**

### SPURS YAJITOSA KWA SORO
KLABU ya Tottenham Hotspur inamuwinda kiungo wa Celtic na raia wa Ivory Coast, Ismaila Soro, 22. **(Mail)**

### PROPPER AWINDWA PSV
KIUNGO wa Brighton, Davy Propper mwenye umri wa miaka 29 raia wa Uholanzi, anawindwa na klabu yake ya zamani ya PSV Eindhoven. **(The Argus)**

### LUIZ NA MKATABA ARSENAL
ARSENAL bado haijaanza mazungumzo na mlinzi wa kati wa Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 34, kwa ajili ya kusaini mkataba mpya. **(Evening Standard)**

# GEITA WANAWAKE KUCHAGUANA J'PILI

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Soka cha Wanawake cha Mkoa wa Geita (GWFA), kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu Jumapili wiki hii, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Geita (GEREFA), Pius Kimisha, alisema maandalizi ya uchaguzi huo yamekamilika na wadau wamejitokeza kuwania katika nafasi zote zilizotangazwa.

Kimisha alizitaja nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo kuwa ni mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu, katibu msaidizi, mweka hazina, mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa (TWFA) na wajumbe watatu wa Kamati ya Utendaji.

"Tunatarajia uchaguzi huu utafanyika kama ilivyotangazwa na viongozi watakaochaguliwa wautumikie mpira wa wanawake kwa moyo mmoja, tunaamini wagombea wote wanania ya kuona soka la wanawake Geita linaendelea," alisema Kimisha.

Aliongeza kuwa mchakato wa uchaguzi huo awali ulisimama kwa muda ili kupisha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, lakini sasa kila mmoja yuko tayari kutimiza jukumu hilo la kidemokrasia.

Mikoa 21 ya Tanzania Bara imeshafanya uchaguzi kwa ajili ya kupata wawakilishi watakaoshiriki kwenye uchaguzi wa Chama cha Soka cha Taifa (TWFA), utakaofanyika baadaye mwaka huu.

# KMC FC KAMILI KUIFUATA DODOMA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa KMC FC umesema kikosi chao kipo tayari na imara kuwafuata wenyeji wao Dodoma Jiji FC kwa ajili ya mechi ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

KMC ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Kurugenzi FC ya Simiyu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa KMC FC, Christina Mwagala, alisema wachezaji wake wameendelea kufanya mazoezi maalumu ili kuwajenga vema nyota wake kwa ajili ya kuimarisha viwango vyao na kukabiliana na ushindani.

Mwagala alisema ndoto zao msimu huu ni kuchukua kombe hilo ili wapate tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa na si kusindikiza timu nyingine.

"Tunajiandaa kwenda kwenye mchezo mgumu ambao kimsingi ukifungwa ndio unakuwa umeaga michuano hiyo, kwakutambua hilo, tunajidhatiti ili kupata matokeo mazuri ambayo yatatupa fursa ya kuendelea mbele kwa sababu KMC FC tunalihitaji kombe hilo kwa umuhimu mkubwa sana,"alisema.

# MASTRAIKA LIGI KUU BARA WABURUZWA UFUNGAJI FA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mashindano ya Kombe la FA yakitarajiwa kuingia katika raundi ya tano mwishoni mwa wiki hii, mastraika wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaonekana 'kuburuzwa' katika michuano hiyo na nyota wanaocheza kwenye madaraja ya chini, imefahamika.

Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube, anaongoza kwa kucheka na nyavu akiwa na mabao 12 mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, lakini wachezaji watatu wa madaraja ya chini ndio wanaongoza ufungaji katika michuano ya Kombe la FA.

**Wachezaji hao ni Isack Kuwayawaya na Junius Kangwa wote kutoka Mageraza FC na Benjamin Dominic wa Itezi FC ambao kila mmoja amefunga mabao manne.**

Kwa bahati mbaya sana timu hizo zote zimeshatolewa katika michuano hiyo, hivyo wachezaji hao hawana tena nafasi ya kujiongezea mabao.

Wachezaji wa Ligi Kuu Bara ambao wamefunga mabao mengi kwenye michuano hiyo ni Najimu Magulu wa JKT Tanzania ambaye ana mabao matatu, Anuary Jabir wa Dodoma Jiji FC na Andrew Senchimba wa Ihefu SC mwenye mabao matatu pia. Wengine wenye mabao matatu ni Kankole Hamisi wa Kahama United, Paul Masalu (Chato Stars), Adolf Mpangule (Nyoka FC), Bakari Selemani (Amboni Stars), Joijo Johnson (Kipigwe FC) na Kennedy Bago wa Eagle Stars.

Michuano hiyo itaendelea tena kuanzia kesho Ijumaa hadi Jumapili na timu zitakazoshinda, zitatinga hatua ya robo fainali. Prisons inatarajiwa kuwakaribisha Yanga kesho kwenye Uwanja wa Nelson Mandale mjini Sumbawanga na Jumamosi mabingwa watetezi, Simba watacheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku JKT Tanzania ikiwaalika Namungo.

Kikosi cha Mwadui FC ambacho kinaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, chenyewe kitawakaribisha Coastal Union wakati Rhino Rangers itacheza dhidi ya Arusha FC, Biashara United itawaalika Ruvu Shooting, Polisi Tanzania yenyewe itawafuata Azam FC na Dodoma Jiji watapambana na KMC.

**MAZOEZI...**



Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Msimbazi Mseto (Katikati), akipiga hesabu ya kuwachambua wachezaji wa Shule ya Msingi Muhimbili, wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Umoja wa Michezo kwa Shule za Msingi katika viwanja vya Michezo vya Jakaya Kikwete, Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Yanga Princess alilia kiwango

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupata ushindi, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake dhidi ya Kigoma Sisterz iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi.

Yanga Princess iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kigoma Sisterz na kuendelea kuwafukuza kileleni watani zao na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba Queens.

Lema aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake hawakuonyesha ubora wao ambao walionyesha katika michezo iliyopita ya mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

Kocha huyo alisema licha ya kupata ushindi, lakini wachezaji wake walikuwa wanapoteza mipira kizembe na kuwapa nafasi wapinzani kutengeneza mashambulizi.

Alisema wachezaji wake hawakuwa na stamina imara na jambo hilo lilichangia pia kucheza mchezo huo chini ya kiwango na kushindwa kutumia vema nafasi mbalimbali walizopata katika mechi hiyo.

"Nina imani hatukustahili kupata ushindi wa mabao haya, tulitakiwa kupata idadi kubwa zaidi ya hayo ili kuendelea kukimbizana na aliyekuwa juu yetu katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hii msimu huu," alisema Edna.

Alisema wana matarajio makubwa ya kuendelea kupambana katika kila mechi ili kutimiza malengo ya kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza.

Yanga Princess wako katika nafasi ya pili wakiwa na pointi 44 huku Simba Queens ikiwa kileleni na alama 45 katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

# Michezo

Jumatano Aprili 28, 2021


Nipashe

Messi aandaliwa ofa nono isiyopingika PSG



HABARI UK.22

PASUA...



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akifurukuta mbele ya msitu wa mabeki wa Dodoma Jiji FC, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara ambayo waliibuka na ushindi wa mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.. **PICHA: SIMBA**

## Tuisila fiti kuibeba Yanga kwa Prisons

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema hauna cha kupoteza kwa sasa na wako fiti kuwavaa Tanzania Prisons na kuibuka na ushindi kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho, maarufu FA Cup.

Kikosi cha Yanga tayari kimeshawasili mjini Sumbawanga kwa ajili ya kuwakabili wenyeji wao hao kwenye mchezo utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Nelson Mandela.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Makipa wa Yanga, Razak Siwa, alisema kikosi chao kipo fiti na wanatarajia kuwapo kwa nyota wao wote akiwamo, Tuisila Kisinda aliyekuwa majeruhi ambaye sasa yupo fiti kurejea uwanjani kuipambania timu.

Alisema Kisinda yuko fiti na miongoni mwa wachezaji waliokuwapo kwenye mipango ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, hawatarajii kupoteza mechi dhidi ya Tanzania Prisons.

"Tunapambana katika vita vya ubingwa wa Ligi Kuu, lakini pia tunahitaji kufanya vizuri katika Kombe la FA, muhimu kwetu kushinda dhidi ya Tanzania Prisons kwa ili tuendelee kuwapo kwenye malengo yetu ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

"Tumeona upungufu wetu kwenye mechi dhidi ya Azam FC, safu ya ushambuliaji inapaswa kuwa na utulivu na kuhakikisha tunatumia vizuri nafasi tunazotengeneza uwanjani," alisema kocha huyo wa makipa.

Wakati huo huo beki wa kati Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja', anatarajiwa kuungana na kikosi cha timu hiyo baada ya kumaliza msiba wa dada yake.

Beki huyo hakuwa kwenye msafara wa kikosi cha timu hiyo kilichoondoka juzi, Aprili 27, kutokana na matatizo ya kifamilia.

# GOMES AHESABU BINGWA SIMBA

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Kujitoa na morali wa wachezaji kwazidi kumpa jeuri huku akieleza sasa wanahitaji...

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema ushindi kwenye mechi dhidi ya Dodoma Jiji FC juzi, ulikuwa muhimu zaidi kwao kwa sababu umesababisha kuweka pengo la pointi nne kati yao na timu inayoshika nafasi ya pili, hivyo sasa anaweza kusema kuwa anaukaribia ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza baada ya mechi dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambayo timu yake iliibuka na ushindi wa mabao 3-1, alisema wamecheza mechi tano kwa siku zisizozidi 15, huku mchezo wa juzi ukichezwa siku tatu tu baada ya mechi dhidi Gwambina, hivyo anaona vijana wake walijitahidi sana kwa sababu walicheza wakiwa na uchovu mkubwa.

"Ilikuwa mechi muhimu. Tulicheza siku tatu baada ya mechi ya ugenini ambayo tulishinda na ilikuwa muhimu kushinda ili kuweka tofauti kubwa ya pointi kati yetu na wanaofuata.

"Tulicheza tukiwa na uchovu kwa sababu tulikuwa tumecheza mechi tano kwa siku ambazo hazizidi 15, lakini tumeshinda zote, ni jambo la kujipongeza na inatufanya tuwe kwenye hali nzuri ya kuukaribia ubingwa," alisema Gomes.

Kocha huyo aliongeza kuwa, walistahili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo kutokana na wachezaji wake kupambana na kujitoa uwanjani kutafuta pointi tatu dhidi ya Dodoma Jiji FC.

"Dodoma Jiji FC walianza vizuri kipindi cha kwanza na kupata bao la kusawazisha, hii inatokana na uchovu wa wachezaji wangu baada ya majukumu makubwa ya kutafuta pointi tisa Kanda ya Ziwa, nawapongeza wachezaji kipindi cha pili tulibadilika na kutumia nafasi vizuri na kuibuka na ushindi huo," alisema Gomes.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata, alikiri wapinzani wao kuwa bora zaidi hususan kipindi cha kwanza kwa kutumia vema nafasi walizozipata licha ya kufanikiwa kutoka sare ya bao 1-1 dakika 45 za kwanza.

"Mchezo ulikuwa mzuri kwa pande zote mbili hasa dakika 45 za kipindi cha kwanza, niwapongeze Simba kuwa na kikosi imara na kuweza kubadilisha matokeo kipindi cha pili baada ya wachezaji wangu kukosa kujiamini na kuwapa nafasi washambuliaji wa timu pinzani kutufunga mabao mawili," alisema Makata.

Simba kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 61 na viporo viwili mkononi huku Yanga iliyopo mbele michezo miwili ikishika nafasi ya pili kwa alama zake 57, zilizotokana na mechi 27.

Timu hizo zitashuka dimbani keshokutwa, Jumamosi kwenye mechi za raundi ya 16-bora ya Kombe la FA, Simba ikiikaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Yanga ikiwa ugenini katika Dimba la Nelson Mandela mjini Sumbawanga dhidi ya Tanzania Prisons.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >